# Nipashe

**JUMAPILI**

Jumapili Desemba 17, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581527

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 9

UKURASA 2

**DED** na mhandisi matatani mil. 500/- za ujenzi hospitali



UKURASA 3

**Bil.** 4.9/- zatolewa kwa waathirika mafuriko Katesh



UKURASA 17

**Majeshi** Israel yaua mateka watatu Gaza

# Rais Samia ashangazwa viwango duni vya wahitimu



• **Asema** wanapoingia kwenye ajira wanaonyesha uwezo mdogo, aagiza... *Endelea Ukurasa 2*

## KKKT yaanzisha huduma maalum kwa wafungwa magerezani

UKURASA 3



RIPOTI YA UCHUNGUZI

## Vyakula vya stendi, barabarani vyaweka hatarini afya za walaji

UKURASA 4


**MICHEZO** VAR RASMI KUTUMIKA LIGI KUU BARA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mkurugenzi, mhandisi matatani mil. 500/- za ujenzi wa hospitali

**Na Augusta Njoji,** MULEBA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ametoa siku nne kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya Muleba mkoani Kagera Elias Kayandabila (ambaye sasa ni Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora) na Mhandisi Zefania Chacha kutoa maelezo ya kwa nini fedha zilizotengwa Sh. milioni 500 zimeshindwa kukamilisha majengo ya hospitali ya wilaya hiyo.

Pia ametoa mwezi mmoja kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Dk. Peter Nyanja, kukamilisha majengo ya hospitali hiyo.

Akizungumza jana baada ya kutembelea hospitali hiyo, Mchengerwa alisema Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilitoa Sh. milioni 500 kwa kila halmashauri isiyo na hospitali ya wilaya kwa ajili ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa majengo ya wagonjwa wa nje na maabara.

"Inashangaza kuwa serikali inatoa fedha kwa ajili ya miradi lakini baadhi ya watumishi wanazitumia ndivyo sivyo. Hata kama mkurugenzi amehama kituo cha kazi lazima atoe maelezo na yafike ofisini kwangu Jumatano ijayo.

"Haiwezekani Rais Samia (Suluhu Hassan) awaletee wananchi wake fedha za kuwajengea hospitali lakini wengine wanazitumia vibaya. Hiyo haiwezekani na wala sitakubali hali kama hiyo,"alisema.

Aidha, aliutaka uongozi wa halmashauri hiyo kutumia mapato ya ndani kukamilisha ujenzi wa majengo ya wagonjwa wa nje na maabara ili wananchi waanze kupata huduma wakati majengo mengine ya wanamalizia.

"Mkurugenzi hakikisha unamaliza ujenzi wa majengo haya na kuwa ifikapo Januari nitakuja kukagua. Nendeni mkafanye mapitio ya bajeti zenu, hakikisheni mnatenga fedha ujenzi ukamilike Januari ili wananchi wapate huduma nikija kukuta kinyume chake nitakusimamisha na kupeleka jina lako kwa Mheshimiwa Rais ili akutengue,"alisema.

Alisema fedha ambazo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliahidi ya Sh. bilioni moja serikali itazileta Januari, mwakani na kuwa zitatumika kujenga majengo mengine ya hospitali.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatuma Mwassa, alisema kuna usimamizi dhaifu wa miradi kwenye halmashauri hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Dk. Abel Mwendawile, alisema tayari walishaielekeza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupitia gharama za ujenzi wa hospitali hiyo.

Alisema ili kukamilisha majengo hayo kiasi cha Sh. milioni 191.9 zinahitajika na kuahidi kuzitafuta wakati wa kufanya mapitio ya Bajeti ya mwaka 2023/24.



Mufti Mkuu wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubeir, akizungumza baada ya vijana 20 wa Kiislamu kufungishwa ndoa katika Msikiti wa Mohamad Saadis Bakwata, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Samia ashtushwa uwezo duni wahitimu

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameshtushwa na ubora wa wahitimu wa taasisi mbalimbali za elimu ya juu nchini katika soko la ajira akibainisha kuwa wakiingia kazini utendaji wao ni duni, hivyo kuibua maswali kuhusu ubora wa elimu nchini.

Aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 50 ya Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) sambamba na uzinduzi wa kitabu kinachoelezea historia ya baraza hilo.

Rais alisema bila ya kuwa na upimaji unaozingatia haki, ni vigumu kuzalisha ajira zenye tija kwa karne hii. Ili kuendana na malengo waliyojiwekea, upimaji unaozingatia haki utasaidia kupatikana kwa nguvu kazi sahihi na yenye uwezo katika soko la ajira na kwa manufaa ya taifa.

"Leo hii tuna wahitimu mamilioni kutoka vyuoni. Ninadhani kuna Vice Chancellors (makamu wakuu) wa vyuo. Tuna wahitimu kwa mamilioni na maelfu wanatoka vyuoni, tunapowachukua ndani ya ajira, wakipewa hata kazi ndogo hawawezi.

"Unajiuliza huyu kaja na cheti chake katoka chuo? kafundishwa chuo? Lakini hili hawezi kufanya sasa tunazalisha nguvu kazi ambayo haina tija kwa taifa, lazima tujitizame kwenye utungaji mitihani na usahihishaji wa mitihani.

"Kubwa zaidi, udhibiti wa mitihani. Tumetoka vyuoni, wote tumepita huko tunajua yanayoendelea huko. Sasa tukitoa mianya ya watoto kufanya mitihani kwa kuijua kabla au kupenyeza mitihani, tunazalisha watu ambao hawako sawa kichwani, hawakupikwa na kuiva vizuri vichwani," alisema.

Rais alisisitiza kuwa kutoka darasani si kufanya kazi wanazotakiwa bali wanahitaji mafunzo na mtu awe vizuri kufuata anachofundishwa.

**MWAROBAINI UDANGANYIFU**

Rais Samia alisema jana alizindua mnara wa kumbukumbu wenye kaulimbiu inayosema 'Haki, Uwajibikaji na Ufanisi' na kukumbusha baraza kutenda haki huku akisisitiza udanganyifu wa mitihani utafutiwe mwarobaini katika hatua zote.

"Kama si ndani ya baraza, hata kule kwenye kamati za mitihani basi iende ikatafutiwe suluhu yake. Kuizungumzia ni hatua moja, kuchukua hatua kuhakikisha haipo ni hatua nyingine.

"Profesa (Adolf) Mkenda (Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia), usiogope kulaumiwa. Lawama tunazo tu chukua hatua, simama kweli kweli na si kwenye mitihani tu, maeneo yote lawama zipo.

"Na ukiona unalaumiwa unafanya vizuri. Usipofanya vizuri watu wanasema chini chini mmmh! Wala hafanyi vizuri. Ukiona watu wanasimama wanakulaumu, ujue mambo yako super (upo vizuri) endelea.

Pia alilitaka baraza kutunza vifaa na mitambo iliyopo na kuahidi katika bajeti zijazo, utaongezwa mtambo mmoja kila mwaka ili ifikie mitatu na kila mmoja unagharimu Sh. bilioni sita.

Rais Samia alisema katika kufanya mazingira yafanane, serikali inapambana kupeleka umeme vijijini na kufanya masomo ya sayansi kwa mtandao jambo ambalo limeanza kutoa matokeo chanya kwa baadhi ya wilaya zilizofungiwa.

"Waziri wa Elimu ushikane na Waziri Nape (Nnauye) Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari mwangalie gharama zinazohitajika kwa shule zilizo mbali lakini umeme upo," aliagiza.

**MSONGAMANO MA DARASANI**

Rais Samia alisema alikuwa anaangalia kituo cha runinga cha TBC na kuona shule moja iliyoko Nyamagana, Mwanza ikiwa na idadi kubwa ya wanafunzi darasani na kuhoji halmashauri husika ilishindwa nini kuona hilo ili kupeleka madarasa.

Alisema pamoja na jitihada kubwa zinazofanyika ikiwamo ujenzi wa madarasa, bado serikali ina mzigo mkubwa wa kuwekeza katika miundombinu ya elimu.

Ongezeko la wanafunzi, alisema linachangiwa pia na sera ya msisitizo ya kuhakikisha kila mtoto anapata fursa ya elimu, ambalo ni agizo kwenye Dira ya Maendeleo ya Miaka 25 kutoka mwaka 2000 hadi 2025.

Alisema pamoja na mageuzi mazuri yanayofanywa na Wizara, inabidi kuwe na utaratibu wa mageuzi ya sera na utekelezaji wake kuanzia mtoto anaposajiliwa, anapokaa darasani, njia za kufundisha, walimu na dhana za kufundishia na utaratibu wa elimu.

Rais alisema mwaka 1973 baraza lilipoanzishwa lilisajili watahiniwa kidato cha sita 2,834 na mwaka 2023 wamefikia 106,883 na kidato cha nne kutoka watahiniwa 12,714 hadi 572,338 na shule za msingi walikuwa 106,203 na sasa ni milioni 1.397.

"Ni dhahiri idadi hii itaendelea kuongezeka siku hadi siku, hivyo kulazimisha uwekezaji mkubwa ambao serikali inapaswa kuufanya katika sekta ya elimu hususani ujenzi wa shule na miundombinu," alisema.

Waziri Mkenda alisema katika kutekeleza sera ya elimu ufanyaji wa mitihani utaangaliwa zaidi.

"Moja ni mafunzo ya amali. wamekubaliana mtu akiingia kidato cha kwanza akifika kidato cha nne, atapata cheti kinachoitwa Cheti cha VETA vinavyotolewa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi (NACTVET) inakwenda kwa utaratibu ambao ni tofauti na NECTA. Tutaainisha juhudi hizi, tutaanza kidogo alafu tutaongeza kasi mbele," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema umefika wakati wanaopata daraja sifuri mtihani wa kidato cha nne, waanze kutambuliwa na kufanyiwa utafiti.

# HABARI KITAIFA

## Bil. 4.9/- zachangwa msaada mafuriko Katesh

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema mpaka jana kiwango cha fedha kilichokusanywa baada ya maafa ya mafuriko na maporomoko ya tope Mji mdogo wa Katesh, wilayani Hanang, mkoani Manyara, kimefikia Sh. bilioni 4. 953.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi wa Idara ya habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, mpaka sasa hakuna miili zaidi iliyoopolewa.

Akichanganua kiasi hicho, alisema mpaka sasa fedha zinazoendelea kukusanywa kutoka kwa wananchi, kampuni na taasisi mbalimbali kupitia akaunti ya Mfuko wa Taifa wa Misaada ya Maafa ni Sh. milioni 218.9.

Alisema fedha zinazokusanywa na taasisi na mashirika ya umma kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina hadi sasa zimefikia Sh. bilioni 2.234.

"Jumla kuu ya fedha zote zilizokusanywa kutokana na maafa haya zikichanganywa na za wahisani mbalimbali wa nje Sh. bilioni 2.5 tumefikisha Sh. bilioni 4.953 mpaka sasa," alisema.

Pia alisema serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Halmashauri ya Hanang zinaendelea kupokea misaada ya chakula, vitu na vifaa mbalimbali kutoka kwa makundi mbalimbali ndani na nje ya nchi ambapo hadi sasa kwa thamani ya soko ni Sh. bilioni 2.182.

Aidha, alisema kampeni ya huduma za afya, jumla ya kaya 6,640 wilayani humo, zimefikiwa na wataalam wa afya na kupatiwa vidonge 225,975 vya kutibia maji.

Aidha, alisema hakuna tatizo la magonjwa ya mlipuko kama kuhara au kipindupindu. "Kwa kutumia wataalam wa Wizara ya Afya ambao ni wauguzi wawili na madaktari bingwa watatu wa afya ya akili wakiwa na maofisa ustawi wa jamii 91 kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, mpaka sasa jumla ya waathirika 2,496 wamepatiwa huduma za afya ya akili na kisaikolojia," alisema.

Alisema miili 87 kati ya 89 imetambuliwa na kuchukuliwa na ndugu kwa ajili ya maziko, majeruhi wamebaki wanane kati ya 139 waliokuwapo hospitalini na wathirika 30 kutoka kaya 12 ndiyo wamebaki kambini.



Wafanyabiashara katika kituo cha mabasi Pugu jijini Dar es Salaam wakiwa wamepanga bidhaa zao kusubiri wateja jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KKKT yaanzisha huduma wafungwa magerezani

**Na Halfani Chusi**

KANISA la kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, imeanzisha huduma maalum kwa wafungwa katika magereza ya Ukonga na Segerea jijini Dar es Salaam.

Uzinduzi rasmi wa huduma hizo ulifanyika katika ibada zilizofanyika katika sharika za dayosisi hiyo za Ukonga na Segerea na baadaye katika magereza hayo.

Akizungumza wakati wa ibada katika Usharika wa Segerea, Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Alex Malasusa, alisema huduma hizo zinalenga kuwasaidia na kuwatia moyo wafungwa ili wasijione wapweke.

Alisema wafungwa ni sawa na watu wengine lakini kinachowatofautisha ni sehemu walipo, hivyo wanahitaji kupewa misaada na kuonyeshwa upendo kwa kupatiwa misaada ya kibinadamu na huduma za ibada.

Huduma watakazopewa wafungwa hao ni ibada za mara kwa mara zikiwamo za kila Jumapili, misaada ya kijamii na kibinadamu pamoja na ushauri nasaha. Askofu Malasusa alisema huduma hizo zitasimamiwa na wachungaji viongozi wa sharika za Segerea na Ukonga ambako magereza hayo yako.

Askofu Dk. Malasusa ambaye pia ni Mkuu Mteule wa KKKT, aliwaahidi wafungwa gerezani kuwatafutia mawakili ili kuangalia namna ya kuwasaidia katika kesi mbalimbali zinazowakabili ikiwamo kukata rufani pale inapowezekana.

Dk. Malasusa alisema wafungwa ni kundi muhimu ambalo linatakiwa kuangaliwa kwa jicho la namna ya kipekee kwa kuwa wanapopata huduma zikiwamo za kiibada, wengi wao wana uwezo wa kubadilika na kuwa raia wema.

"Tulipofika pale Ukonga tulisikia sauti kubwa wanaimba nyimbo, kuna kwaya kubwa sana. Kwa kweli wanahitaji ibada za mara kwa mara ili wajione ni watu kama wengine. Ni imani kwamba huduma hizi zinaweza kuwabadili baadhi na kuwa wema na wengine wanajutia makosa waliyoyafanya.

"Wakati tunakwenda pale nilipata ushauri kwamba tusiwahubirie habari za makosa yao bali tuwahubirie upendo. Kwa kweli wamefarijika sana kwani wameshiriki meza ya Bwana (Sakramenti), wamepata kipaimara na wengine wamebatizwa. Tuliposema tunabatiza tulidhani ni wale wachache waliokuwa wameandaliwa kumbe kulikuwa na wengi waliohitaji huduma ile na tumewabatiza," alisema.

Akiwa ndani ya magereza ya Ukonga na Segerea, Askofu Dk. Malasusa aliongoza ibada kuwaombea wafungwa na kushiriki nao katika sakramenti ya Meza ya Bwana huku akihimiza amani, ushirikiano na kuwataka wafungwa kumuomba Mungu bila kujali wako wapi kwa kuwa yeye yuko mahali popote.

"Endeleeni kumwomba Mungu na kutuombea sisi viongozi wa dini, ili tuendelee kukumbuka kuwaombea ili serikali na vyombo vya uamuzi viweze kuwasamehe," alisema Askofu Malasusa akiwa ndani ya gereza la Segerea na kuibua shangwe kutoka kwa wafungwa.

Awali, wafungwa waliomba kusaidiwa biblia, kinanda, vitabu vya dini, mawakili wa kuwasaidia katika kesi zinazowakabili na huduma ya maombi ambapo Askofu Malasusa aliahidi kuwasaidia kwa kushirikiana na wadau wengine.

"Nimefurahi sana nilipokuwa ninaingia humu ndani, nimekuta mnamwabudu Mungu, mnaimba nyimbo za dini na kucheza, hii inaonyesha ni jinsi gani mnajua uwapo wake.

"Kuhusu maombi yenu tutayatatua yale ambayo yapo ndani ya uwezo wetu, na mengine tutashirikiana na wadau wengine," aliahidi Askofu Malasusa.

Awali, Askofu Malasusa, akiwa katika Usharika wa Segerea, aliongoza ibada ya kuwaombea askari magereza na kuzindua huduma ya utolewaji wa huduma ya kiroho kwa wafungwa waliopo gerezani ambayo ilikuwa haitolewi.

Dk. Malasusa aliwataka viongozi na waumini wa kanisa hilo kuwaombea pia maofisa na askari Magereza kutokana na kazi kubwa wanayofanya ya kuwatunza na kuwasimamia wafungwa.

"Hawa watu wanastahili pongezi na kuwaombea. Wao ni tofauti na sisi viongozi wa dini ambao watu wanakuja kwa kusikia kengele lakini wao wanapelekewa watu wakiwa kwenye magari na wengine wamefungwa pingu," alisisitiza.

Mkuu wa Gereza la Segerea, Dastan Lissu, alimshukuru Askofu Malasusa kwa kulikumbuka gereza hilo pamoja na kumteua Mchungaji atakayekuwa anakwenda kuongoza ibada.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ANNE BAKUNAME JAMES** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 668 DPG – TOYOTA IST.** Chassis namba **NCP600215693.** Engine namba **2NZ3630225.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/55255/2023.**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**SABINA CHARLES MWILONGO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA S0683/0013 KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA KALENGA SEKONDARI MWAKA 1995. YEYOTE ATAEFANIKIWA KUKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU. NAE POLISI TAARIFA: **PHQ/PWA/MKU/4766/2023.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 26189 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE CHARLES ISDORI MLOKA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY:-**
**SESILIA CHARLES KILEGU**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 21 day of 12/2023

**DATED at MOROGORO this 04th day of DEC 2023**

**Resident Magistrate**

**3FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 25952 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE OPPORTUNA NEWA KANGWA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY VERONICA ERNEST KANGWA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above – named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 18th day of DECEMBER, 2023.

DATED at DAR ES SALAAM this 23rd day of NOVEMBER, 2023.

*Senior Resident Magistrate*

RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Vyakula vya stendi, barabarani vyaweka hatarini afya za walaji

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KUNA msemo, 'ukimchunguza sana bata huwezi kumla', ukiwa na tafsiri kwamba kuna baadhi ya vitu ukivifanyia udadisi namna vilivyo au vinavyotengenezwa, huwezi kuvitumia.

Lakini hili haitoi uhalali wa kinachoshuhudiwa kwa vyakula wanavyouziwa abiria wanaotumia Stendi Kuu ya Mabasi Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Mwandishi wa habari hizi, baada ya kufuatilia kuanzia uandaaji wa vyakula hivyo hadi vinavyofungashwa, amebaini dosari ambazo si tu zinakiuka miongozo na kanuni za afya, bali pia zinakinzana na maelekezo ya Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009.

Sheria hiyo katika kifungu cha 32, inaelekeza mfanyabiashara anapotaka kutoa huduma ya chakula, sharti awe na eneo la kuhifadhi chakula lenye ukubwa wa kutosha, lisitunze unyevu, pawe na mwanga wa kutosha, penye kupitisha, pawe safi na pasiwe na wadudu wavamizi, pasiwe karibu na msalani, pawe na sakafu, kuta na dari zinazosafishika.

Hata hivyo, kilichobainika Moshi, vyakula vinaandaliwa mazingira hatarishi yanayojumuisha maeneo ya karibu na msalani, mifereji ya maji machafu na dampo.

Vinakouzwa vyakula hivyo ni katika eneo la Stendi Kuu ya Mabasi Moshi na vichochoro vya kuingia katika stendi hiyo inayotumiwa na wastani wa watu 1,000 kwa siku kwa mwezi Februari hadi Oktoba na wastani wa watu 3,000 kwa mwezi Novemba hadi Januari.

Mfanyabiashara wa nguo jijini Arusha ambaye mara kwa mara hupita katika Stendi Kuu ya Mabasi Moshi, Jonathan Mchomvu, anasema amekuwa shuhuda wa abiria wengi kukumbana na maradhi ya tumbo wawapo safarini kutokana na kula vyakula vinavyoandaliwa katika mazingira hatarishi.

"Mimi binafsi ni miongoni mwa abiria waliopata madhara baada ya kununua mishikaki katika eneo la pembezoni mwa lango kuu kutokea hapa stendi.

"Shida hii ya vyakula vya aina hii haipo hapa Moshi pekee. Hata Stendi Kuu ya Arusha na Dar es Salama kuna tatizo hili. Kuna siku nilichukua keki zinazopitishwa kwenye magari kule Arusha, ilinisababishia shida ya tumbo. Kwa sasa nimejitambua, ninatembea na dawa za tumbo," anasema Mchomvu.

Abiria mwingine Ester Elinathani aliyezungumza na mwandishi katika Stendi Kuu ya Moshi wakati akiwa safari



Moja ya maeneo kunakoandaliwa na kuuzwa chakula katika uchochoro River Nile, ambapo maji machafu yanapita. **PICHA: MWANDISHI WETU**

kwenda Morogoro, anatoa angalizo kwa walaji wa vyakula hivyo, vingi haviandaliwi katika mazingira salama kiafya, hata uhifadhi wake unatia shaka.

Hata hivyo, Ester anasema wengi wa walaji wa vyakula hivyo, kipato chao kiko chini. Hawawezi kununua vyakula katika hoteli ambazo wamiliki wa mabasi wameingia nazo ubia kupitisha abiria wao huko.

"Uchumi umekuwa mgumu sana. Mtu anatoka nyumbani kwenda msibani au katika utafutaji wa maisha, hawezi kuacha kununua sambusa ya Sh. 500 akanunua ya Sh. 1,000 au akaacha kununua chakula cha 'buku jero' (Sh. 1,500) akanunue cha Sh. 7,000," anafafanua Ester, mkazi wa Njoro, Manispaa ya Moshi.

Shabani Mzava ni dereva wa basi linalofanya safari za Moshi-Arusha. Anasema: "vyakula hivi vinaandaliwa katika mazingira ambayo wakati mwingine tunamwachia Mungu tu.

"Sambusa zinapikwa Kibosho, Marangu, Njoro Pasua na Mailisita huko. Anapewa kijana, analeta hapa stendi (Moshi) kuuza na zikibaki anazirudisha, kesho zitauzwa tena, zikibaki keshokutwa zitaendelea kuuzwa.

"Kula sambusa iliyochacha ni jambo la kawaida tu. Hawa wanaouza keki wakati mwingine haziivi, zimeharibika, basi tu kwa kuwa umeshauziwa unapotezea, lakini kwa kweli Kilimanjaro hakuna uongozi unaosimania afya za watu," analalama.

Mfanyabiashara wa simu katika stendi hiyo, Hamad Mzee, anasema hali mbaya zaidi kwa vitafunwa wanavyouziwa kutokana na kuandaliwa katika mazingira machafu karibu na stendi.

"Ninaona vituo vingi vya afya vinajengwa. Kama uuzaji wa vyakula vya aina hii vitaendelea katika stendi na maeneo mengi yenye mkusanyiko wa watu, vituo hivyo vya afya havitakosa wateja.

"Ukipita katika stendi, pembezoni mwa eneo wanalokaa polisi wa usalama barabarani ni moja kati ya maeneo ambayo yanaandaliwa chakula katika mazingira machafu, kuna mitaro ya maji machafu na watu wanaandaa chakula hukohuko na kuwapatia wateja.

"Ikiwa mamlaka zipo zinaangalia tu, wapishi wana nguo chafu, vyombo vyao havioshwi kwa sabuni, mvua ikinyesha kunakuwa na uwezekano wa kupata magonjwa ya mlipuko," anasema Mzee.

Wakala wa mitandao ya simu katika stendi hiyo, Zuhura Bakari, anasema kuwa mbali na wauzaji hao, wapo wanaopika vyakula nyumbani kisha kupeleka katika stendi hiyo na kuviuza. Hawafuati kanuni za afya zinazowataka kuweka chakula katika eneo safi, watoa huduma kufunika vichwa vyao na kuvaa sare maalum.

Eva Munisi, muuzaji dawa katika duka la dawa lililoko katika Stendi Kuu ya Mabasi Moshi, anasema dawa za kuzuia kuhara zinaongoza kwa mauzo dukani. Anabainisha kuwa kwa siku ni kawaida kwake kuuza dozi zaidi ya 30 hasa asubuhi na mchana. Wengi hufika dukani wakilalamikia kuumwa tumbo au kuhara.

Hata hivyo, hairuhusiwi kumuuzia dawa mteja pasipo kuwapo na maelekezo ya daktari.

### WAUZAJI VYAKULA

Mmoja wa wauzaji chakula katika stendi hiyo, Hamida Jumaa, anasema bidhaa zake huziandaa nyumbani kwake Njoro, Manispaa ya Moshi, akitumia nishati ya kuni au mkaa.

"Wako wengine kweli wanapika kwenye mazingira ambayo hayaridhishi, na hawazingatii usafi. Hii ni kutokana na mamlaka za serikali kuanzia ngazi ya mtaa zinatilia mkazo kuchukua fedha tu bila kufanya ukaguzi.

"Wapo wateja wanaokuja na kusema wameona nzi, mende na hata nywele kwenye vyakula ikiwamo mchuzi na uji kwa baadhi ya wafanyabiashara wenzangu," anasema Hamida.

Mfanyabiashara wa sambusa katika stendi hiyo, Samson Isaya, anasema wanalazimika kuuza bidhaa hizo bila kujali usalama wake kiafya kwa wateja ili wapate fedha.

"Bosi anatengeneza nyumbani kwake, anakupa wewe kwa idadi unayoweza kubeba. Unakuja hapa stendi kuuza, jioni unapewa Sh. 3,000. "Sambusa ikianguka chini, hauwezi kuiacha, ni lazima kuifuta na kuirudisha kwenye kindoo chake ili baadaye ulipwe ujira kamili kulingana na makubaliano.

"Ni kweli mazingira hayaridhishi, lakini tutafanyaje? Tupo hapa kusaka kipato. Sambusa zisiponunuliwa zote, hatupewi fedha yote, hivyo itakulazimu kuuza hadi zitakapoisha. Kwa sasa hali ni ngumu, sambusa zinakwenda hadi siku tatu bila mafanikio, ndiyo maana wapo wanaolalamika zimechacha," anafafanua.

Mfanyabiashara mwingine katika stendi hiyo, Zenobia Mgaya, anasema, "ninauza chakula, ninaandaa keki na sambusa na kuleta hapa maeneo ya stendi kwa mwaka wa tisa sasa.

"Ukaguzi upo lakini tuna mbinu tunavyomalizana nao ili na sisi tupate riziki. Haitatokea kumwaga chakula hata siku moja, nitakihifadhi na kukiuza kesho yake. Si mimi tu, bali pia hata wenzangu.

"Tuna mitaji ya tia maji tia maji (midogo), wengi wametelekezewa watoto au kufiwa na waume. Tunasomesha, majukumu ni mengi. Chakula tunapika kwenye mazingira ya kawaida, vyakula vyote vyenye nyama ni Sh. 1,500, vya maharage Sh. 1,000, vyenye samaki Sh. 2,000 hadi 2,500," anasema pasi na shaka, bila kufahamu kwamba kuwa na majukumu mengi hakutoi uhalali wa kuvunja sheria na kanuni za usalama kiafya.

### MADEREVA WALONGA

Mmoja wa madereva wa mabasi wanaopita katika stendi hiyo, Ruben Mfoi, anasema katika safari zao za kusafirisha abiria, kumekuwa na changamoto ya abiria kuhara wakiwa safarini.

"Watu kuugua matumbo ni kawaida wawapo barabarani na hii ni kutokana na aina ya vyakula wanavyotumia. Mwezi Februari, mwaka huu, kuna mtu tulimwacha katika Hospitali ya Same. Tulitoka naye Kibosho lakini kwa bahati mbaya tuliporudi tulijulishwa alipoteza maisha. Sasa hatujui ni kutokana na hali hiyo ya vyakula vya njiani au alikuwa na maradhi mengine," anasema.

Dereva huyo anasema wamekuwa wanakabiliwa na adha ya kusimama mara kwa mara njiani kutokana matatizo yanayowakumba abiria njiani, yakiwamo maradhi ya tumbo na kuhara.

Dereva mwingine wa basi, Harrison Mnzava, anasema kuna haja viongozi kuanzia ngazi ya mtaa hadi kitaifa kuwajibika kwa kushindwa kutekeleza wajibu wao wa kudhibiti uuzaji huo holela wa vyakula.

"Mara kwa mara inatulazimu kusubiria abiria wanaokumbana na tatizo la kuhara. Ukifuatilia, unagundua walinunulia vyakula huko stendi na kuvila. Sisi tunashauri abiria wachukue chakula kwenye maeneo rasmi kwa huduma hiyo, lakini tatizo hili ni kubwa. Wenye mamlaka wamelala usingizi wa pono," anasema.

Katika uchunguzi wake ulioanza Machi, mwaka huu, kwenye maeneo ya Njoro, Pasua, Mboya, Majengo na vichochoro vya mjini Moshi, mwandishi wa habari hii alibaini kuwa kati ya waandaaji 39 wa vyakula aliowafikia, 32 wako katika mazingira yanayokinzana na sheria na miongozo ya kiafya iliyobainishwa hapo juu.

Mwandishi pia alizungumza na wauzaji 24 wa vyakula katika stendi hiyo na maeneo ya jirani. 20 kati yao walikuwa wamefungasha vyakula vyao kwa kutumia vyombo vya plastiki na wengine waliosalia walitumia vikapu

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# ICTC, taasisi ya Ruge kuinua vijana na Wanawake kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICTC) imetia saini hati ya makubaliano na ushirikiano na Taasisi ya Ruge Mutahaba ya kuinua vijana na wanawake kushiriki na kunufaika kiuchumi kupitia matumizi ya teknolojia za kidijitali.

Makubaliano hayo yamelenga kushughulikia maeneo ya utafiti, ukuzaji ujuzi na ubunifu kupitia mafunzo, warsha na mikutano.

Makubaliano hayo yalitiwa saini juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa ICTC, Dk. Nkundwe Mwasaga, na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Ruge Mutahaba, Cynthia Bavo.

Dk. Mwasaga alisema ICTC imefikia makubaliano kwa lengo la kuwawezesha makundi hayo kuwa na uwezo wa kuchangamkia fursa zilizopo katika uchumi wa kidijitali.

Alisema tume iko tayari kutekeleza jukumu walilokubaliana na taasisi ya Ruge Mutahaba kwa kuwa hiyo ni sehemu ya kutekeleza kwa vitendo Sera ya Taifa ya TEHAMA na sera nyingine zinazoitegemea TEHAMA kama nyenzo kuu ya kufikia malengo ya sera husika.

"Kwa hiyo tumeona tuongeze nguvu ya ushirikiano katika kuwainua kisekta wanawake na vijana katika maeneo ya utafiti, ubunifu, na kuwajengea ujuzi na uwezo kwa ujumla kwa njia mbalimbali. "Uchumi wa dunia unakwenda kushikwa na sekta ya TEHAMA, hivyo ni vyema wanawake na vijana wakaandaliwa vyema katika eneo husika, kuanzia ubunifu, utafiti na kadhalika," alisema Dk. Mwasaga.

Bavo ambaye taasisi yake ilianzishwa Juni 22, 2022 kwa lengo la kuendeleza maono ya Ruge Mutahaba ambaye enzi za uhai wake alijikita zaidi katika ustawi wa vijana, wanawake na Watanzania kwa ujumla, alisema wana kila sababu ya kuendeleza mazuri ya Ruge.

Taasisi ya Ruge imejikita katika dhima kuu tano ambazo ni ubunifu, uvumbuzi, umahiri, upambanaji na uzalendo, na ili kutekeleza hayo, inashirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo serikali, sekta binafsi na mashirika ya ndani na ya Kimataifa katika kuendesha miradi ili kutatua changamoto za wanawake na vijana hasa katika eneo la ajira na kutengeneza kipato.

"Enzi za uhai wake, Ruge aliwekeza sana katika ubunifu na ujasiriamali wa vijana na wanawake ili kuwasaidia katika kuinua kipato, hivyo tunalenga kuyapa uhai na kutekeleza maono yake chanya ya kimaendeleo yaliyolenga vijana na wanawake kwa kupitia fursa mbalimbali.

"Taasisi ina mikakati ya kuendesha miradi ya kusaidia wanawake na vijana kupitia ujasiriamali wenye tija, sanaa na ubunifu," alisema.

Mbali na ushirikiano na Taasisi ya Ruge Mutahaba, katika kujenga uwezo na kukuza taaluma ya Tehama nchini, Tume ya Tehama katika mwaka huu wa fedha imejipanga katika kuendelea na ukamilishaji wa vituo vya ubunifu TEHAMA (Soft centers) katika Kanda tano pamoja na kuanzisha kituo kimoja Zanzibar.



Mbunge wa Jimbo la Mbagala jijini Dar es Salaam, Abdallah Chaurembo, akimkabidhi cheti Mjumbe wa Shina namba 39, Ali Bushiri, kutokana na kukitumikia chama hicho vizuri wakati wa Mkutano Mkuu Tawi la Toangoma jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Baraza lataka kasi utangazaji utalii

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI ya Chakula, Kilimo na Utalii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, imesema pamoja kazi kubwa inayofanyika nchini kutangaza sekta ya utalii, bado kuna kazi kubwa zaidi inahitajika kuendeleza sekta hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Hussein Makungu, alisema hayo jana wilayani Bagamoyo wakati wa ziara ya mafunzo ya kamati kujifunza namna Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) inavyoendesha utalii wa ikolojia na malikale katika vivutio vya utalii vya Kaole na Mji Mkongwe wa Bagamoyo.

Makungu alisema Tanzania ina vivutio vingi na kwamba namna miaka inavyozidi kusogea ndivyo idadi kubwa ya watalii inazidi kuongezeka. Kutokana na hali hiyo, alisema kuna haja ya kuongeza juhudi ya kuendeleza zaidi sekta hiyo.

"Utalii si kazi ndogo, tuna kazi kubwa ya kuendeleza utalii. Bado wageni wengi hawajafika Tanzania Bara wala Zanzibar, ila watazidi kuja baadaye. Kwa hiyo inabidi tujipange vizuri zaidi, ninaamini miaka ijayo tutapata idadi kubwa zaidi ya hii tunayoiona sasa maana tuna vivutio vingi.

"Mfano leo (jana) nimesikia historia ya kivutio hiki cha Kaole kilicho chini ya TFS nimevutiwa sana, historia kama hii Zanzibar hatuna lakini hata ukienda Zanzibar nako unakutana na vivutio vingine, hivyo naona tusichoke kuviendeleza na tuzidi kuwa na umoja wa kushirikiana kuendeleza sekta hi muhimu kwa nchi yetu," alisema.

Makungu alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kwa kazi kubwa wanayofanya ya kutangaza utalii duniani.

"Viongozi wetu wanafanya kazi kubwa kutangaza utalii wetu. Mfano kupitia Royal Tour, kazi kubwa imefanyika na dunia nzima imeiona Tanzania na vivutio vyake kwa hiyo tunaomba wasichoke," alisema Makungu.

Mwakilishi wa Tumbe, Pemba, Said Saleh Salim, alisema jambo walilojifunza katika ziara hiyo hususani katika eneo la kivutio cha utalii cha Kaole na Mji Mkongwe wa Bagamoyo, watapeleka na Zanzibar.

Salimu aliwashauri vijana kwenda shule kujifunza masuala ya namna ya kuhifadhi Ikolojia na Malikale kwa kuwa ni miongoni mwa maeneo kulipo na fursa ya ajira.

Mhifadhi Mwandamizi wa TFS, Kelvin Fella, alisema uwekezaji unaofanywa na wakala kwenye ikolojia na malikale ni mkubwa na kwamba lengo kubwa ni kuvutia watalii na hata wanapotembelea kwenye vivutio vyao wafurahie na kutamani kwenda mara kwa mara.

"Tunaweka mazingira namna ambayo mtalii akifika anavutiwa na ikolojia na pia, akifika tumewekeza kumwezesha anapata kila kitu anachokitaka akiwa katika maeneo yetu ya vivutio," alisema Fella.

# Viongozi SACCOS watakiwa kuheshimu katiba

**Na Kulwa Mzee**

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel, amewataka viongozi wa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo cha Mahakama, kufuata sheria, katiba ya chama na miongozo ili wasikivuruge chama.

Prof. Ole Gabriel alisema hayo jana alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mahakama SACCOS uliofanyika katika ukumbi wa Mahakama Kuu.

"Ushauri wangu umegawanyika katika sehemu saba, tufuate sheria, katiba ipo ya chama na miongozo, tusivuruge chama, sehemu ya pili, mikopo inayokopwa irejeshwe ili wengine wakope.

"Tumieni mikopo kwa makusudio uliyokopea, hesabu zifanyike, zikaguliwe na wanachama wapewe taarifa, taarifa ya mwaka iwe inanifikia, iwapo bajeti na mwisho ni vyema kuendesha chama kidijitali," alisema.

Akijibu maombi ya Mahakama SACCOS kuhusu kuongezewa mtaji, alisema mtaji unaombwa kwa ajili ya biashara ihakikishe inarejesha fedha hizo na si kuomba mtaji kwa ajili ya kukopesha.

Alisema maombi ya kuzunguka mikoani kushawishi watumishi kujiunga na chama ameyakataa na kuwashauri kutumia Mahakama Mtandao kuwasiliana na watumishi katika mikoa mbalimbali kwa kuwa, kwa njia hiyo gharama itatumika kidogo na watapata wanachama wengi.

"Maombi ya kupewa vyumba viwili Dodoma na Dar es Salaam hayana shida, nitayashughulikia, leteni nyaraka tuzifanyie kazi, suala la makato ya wanachama linazungumzika, tuweke utaratibu makato yawe yanaingia moja kwa moja kwenye akaunti ya SACCOS,"alisema.

Aidha, Mtendaji Mkuu huyo alitaka sababu tano zinazofanya SACCOS nyingi kufa kuwa ni wanachama kukosa uaminifu na kuwa watu wa majungu, viongozi kukosa ubunifu, mikopo kutorejeshwa, uelewa mdogo kuhusu mikopo na malumbano ya viongozi.

Akisoma hotuba ya chama, Mwenyekiti wa Mahakama SACCOS, Mkufya Matope, alisema ili kuboresha na kuendeleza dhamira nzuri iliyonayo Mahakama SACCOS kwa wanachama wake na watumishi, wanaomba kuongezewa mtaji wa kuweza kuwakopesha wanachama ili waboreshe hali ya maisha ya watumishi.

Mkufya alisema Mahakama SACCOS wanaomba wapewa fursa ya kutumia makongamano, sherehe, mikutano na maonyesho mbalimbali yanayohusu mahakama kuweza kufanya uhamasishaji kwa watumishi wa idara mbalimbali za mahakama wasio wanachama ili waweze kujiunga na chama.

"Tunaomba mwajiri akisadie chama kupata mapema fedha za wanachama zinazotokana na marejesho ya mikopo na mawekezo ya akiba zinazokatwa kupitia mishahara yao kwa kuwa, kuna wakati fedha hizo zinachelewa,"aliomba Matope.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Rais Samia amesema kweli wahusika wachukue hatua

**BARAZA** la taifa la Mitihani Tanzania (NECTA) jana liliadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1973. Katika maadhimisho hayo, Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi na alizungumza masuala kadhaa kwa ajili ya kuboreshwa utendaji kazi wa taasisi hiyo nyeti kwa maendeleo ya taifa.

Rais Samia kwa kiasi kikubwa, alilitaka baraza hilo kubadilika na kuendana na hali halisi ya dunia hususan katika maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari hadi elimu ya juu kwa maana ya vyuo vikuu.

Pamoja na kusisitiza hayo, kubwa ambalo ni mtihani mkubwa kwa NECTA na wadau wote wa maendeleo ya elimu ni kauli ya kiongozi huyo mkuu wa nchi kueleza kushangazwa kwake na viwango duni vya wahitimu katika vyuo vikuu nchini katika soko la ajira. Kwa mujibu wa Rais Samia, uwezo wa wahitimu hao katika kazi wanazozifanya kwa mujibu wa taaluma walizosomea ni mdogo jambo ambayo inaibua maswali mengi kuhusu ubora wa elimu inayotolewa nchini.

Rais alisema hivi sasa kuna maelfu ya wahitimu kutoka katika vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu nchini ambao huhitimu kila mwaka lakini wanapobahatika kupata ajira serikalini na sekta binafsi wanaonyesha udhaifu wa hali ya juu katika utendaji kazi. Hatua hiyo alisema inazua maswali yasiyo na majibu sahihi yakiwamo kama cheti alicho nacho amekipata kihalali.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, ambayo kwa kiwango kikubwa inalalamikiwa na waajiri katika maeneo mbalimbali, aliagiza wakuu wa vyuo na wizara yenye dhamana ya elimu kulishughulikia tatizo hilo kwa kuwa lina athari kubwa katika nyanja zote za maendeleo. Bila kuuma maneno, Rais alisema tatizo hilo haliwezi kuachwa kama lilivyo kwa kuwa taifa haliwezi kuzalisha nguvu kazi isiyo na tija.

Hakika Rais Samia amepasua jipu lililokuwa limeiva kwa muda mrefu lakini lilikuwa limekosa mtu wa kufanya hivyo kwa uwazi. Ni ukweli isiopingika kwamba kiwango cha wahitimu wengi kwa sasa kinatia shaka na hili limekuwa likilalamikiwa na waajiri wengi kutokana na uwezo wao mdogo katika utendaji kazi. Hivi sasa kila fani imekuwa katika matatizo makubwa kutokana na wahitimu kutokuwa na uwezo licha ya kuonyesha kuwa wana ufaulu wa madaraja ya juu.


Ni wakati sasa kwa wizara yenye dhamana ya elimu kukaa na kutafakari kuhusu kauli na maagizo ya Rais kwamba elimu ya Tanzania inatakiwa kufanyiwa mageuzi makubwa ili kuendana na mabadiliko ya sasa ya kidunia ambayo kwa kiasi kikubwa yanatawaliwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kwa ujumla, baadhi ya vyuo na taasisi za elimu ya juu, viko kibiashara zaidi kwa kuonekana vinafaulisha kwa madaraja ya juu ili kuvutia 'wateja' (wanafunzi) kujiunga navyo. Hatua hiyo imesababisha kuwapo kwa wahitimu wenye vyeti safi lakini uwezo wao kikazi ni mdogo.

Lakini pia suala la baadhi ya wanataaluma kuwaonyesha wanafunzi mitihani ama kwa tamaa ya kujipatia fedha au uhusiano wa aina yoyote ile linapaswa kufanyiwa kazi kwa kina. Wako baadhi ya wanataaluma ambao wamekuwa wakidaiwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi, hivyo inakuwa rahisi kuwapatia mitihani na kuikariri ili wafaulu darasani.

Rais ameanika juani hali halisi kuhusu uwezo au viwango duni vinavyoonyeshwa na wahitimu wanaotoka katika vyuo mbalimbali nchini, hivyo ni jukumu la wizara na wadau wake kulifanyia kazi na kulipatia majawabu mujarabu. Ikumbukwe kwamba mzaha mzaha hutumbuka usaha, hivyo suala hilo lipatiwe tiba ya kudumu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Sauti ya Jamii Kipunguni mfano wa kuigwa mapambano dhidi ya ukatili

Na Sabato Kasika

**JITIHADA** za kuleta maendeleo, kwa kawaida zinahitaji kuunganisha nguvu za jamii na serikali ili kufanikisha mipango ya kuwezesha wananchi kusonga mbele na kubadilika kutoka maisha duni kwenda yaliyoimarika.

Katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kuna vikundi kadhaa ambavyo vinajiunganisha nguvu za wanajamii na serikali kuwezesha wananchi kujihudumia kuondoa umaskini na ukatili wa kijinsia.

Hayo ni kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Dar es Salaam, Francisca Makoye, katika mkutano wa mwaka wa maofisa maendeleo ya jamii, iliyofanyika jijini Arusha hivi karibuni.

Katika vikundi vilivyoko Ilala anakitaja Sauti ya Jamii Kipunguni cha Kata ya Kipunguni, kwamba kimeimarika na kujikita katika shughuli za ujasiriamali na hatua hiyo inakwenda sambamba na kutatua changamoto zinazotokana na ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake.

Anaeleza kuwa kimewezesha jamii ya kata hiyo na za jirani za Kitunda na Kivule kufanya shughuli za kiuchumi na kuanzisha klabu za watoto ili kuwalinda dhidi ya vitendo vya ukatili na kuwaendeleza.

Taarifa yake inaendelea kueleza kuwa kituo hicho kimejenga ofisi yenye thamani ya Sh. milioni 11 kupitia vyanzo vyake vya mapato, na sasa ofisi hiyo inatoa msaada wa kisheria, jamii inapata huduma hiyo kwa karibu.

Binafsi ninadhani kwamba, kituo hicho kinafaa kuwa mfano wa kuigwa katika vita dhidi ya ukatili wa kijinsia ndani ya jamii ili kuharakisha jitihada za kukomesha vitendo hivyo nchini.

Historia inaonyesha kuwa kituo hicho kilianzishwa na washiriki wa semina za Jinsia Maendeleo zinazoratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ili kupanua na kuongeza wigo wa kupinga ukatili wa kimwili, kingono, kisaikolojia na kiuchumi.

Hivyo, si vibaya vikundi vingine vikaenda katika ofisi za kituo hicho kujifunza mbinu, ambazo zimekiwezesha kufika hapo kilipo kikiendelea na mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Ikumbukwe kuwa ukatili huo unahusisha ukeketaji katika kata za Kitunda, Kivule na Kipunguni. Mbinu kuu wanayotumia ni uwezeshaji wa jamii kiuchumi, kifikra na pia kuendesha mijadala ya uelewa wa haki.

Aidha, jitihada za kituo hicho zimewezesha kuhudumia watu wengi kuanzia mwaka 2014 ambapo watu 19 walipata huduma mbalimbali, huku mwaka 2016 wakaongezeka hadi kufikia watu 46.

Mwaka 2018 walikuwa 34, ilipofika 2020 walipungua hadi sita na mwaka jana walikuwa wanne, jumla ya waliofikiwa na kupewa huduma mbalimbali ni 109, huku pia kukiwa na mafunzo ya ujasiriamali.

Mafunzo hayo yalianza mwaka 2016 hadi 2023, wanawake waliopata mafunzo ni 2,100, wanaume 510, vijana wa kike 2,700, wa kiume 300, wenye ulemavu wa kike 161 na wa kiume 71, jumla wakiwa ni 5,842.

Katika mafunzo hayo, wahusika walifundishwa mapishi, kilimo rahisi, jinsi ya kusimamia vikundi, saluni, utengenezaji wa urembo na mkaa mbadala na kuanzishwa klabu mbalimbali za kupinga ukatili. Inaelezwa kuwa klabu hizo ni za kupinga ukatili wa kijinsia, ambazo kwa upande wa watoto zipo 30, vijana 30, za wazazi 30 za mabinti wenye watoto 30 na hivyo jumla ya klabu hizo ni 120.

Kimsingi, hatua ya serikali kutambua shughuli za kituo na kukitolea mfano, ninadhani kituo hicho kinajivunia hilo, lakini hakipaswi kujivuna tu bali ni kutumia nafasi hiyo kufanya kazi zake vizuri zaidi.

Elimu ambayo kituo hicho kimetoa ndani ya jamii kuhusu madhara ya vitendo vya ukatili wa kijinsia tangu kianzishwe, ninaamini imesaidia kuwapo kwa klabu za kupinga ukatili huo.

Ushauri wangu ni kwamba, sio vibaya vikundi vingine kujifunza kitu kutoka Kituo cha Sauti Kipunguni na kukifanyia kazi kwani kupata uzoefu kwa wengine ni jambo la kawaida.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# Elimu ya katiba, sheria inahitajika mahakama zitoe haki bila kuombwa



Pascal Mayalla

LEO nianze makala hii kwa kujitambulisha tena kuwa japo mimi Paskali Mayalla ni mwandishi wa habari wa kujitegemea na mtangazaji wa kujitegemea, pia ni mwanasheria na wakili wa kujitegemea. Kwa hiyo kupitia uanasheria wangu, nina mamlaka ya kuikosoa mahakama kwa kutotenda haki.

Nimekuwa nikiandika sana makala kutoa elimu ya Katiba, sheria na haki kupitia safu hii. Safu hii haiishii kuandika tu gazetini bali itakuwa ikirushwa hewani kupitia kipindi cha "Kwa Maslahi ya Taifa" katika runinga mbalimbali. Kipindi cha kwanza ni mahojiano na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Elieza Feleshi kuhusu mahakama zetu kutenda haki.

Siku za nyuma niliandika makala mfululizo za kilio cha haki na miongoni mwa hoja zilizoniibua kumtafuta Jaji Feleshi, ni baada ya moja ya makala hizo kuhoji uwezo wa mahakama zetu kutoa uamuzi wa haki.

Ukosekanaji wa Haki kwenye mhimili wa Mahakama, kunaweza kuwa kunachangiwa na majaji au mahakimu wenye uwezo mdogo kubaini haki?

Hali hii ya mahakama zetu kutotenda haki kwa kitu kinachoitwa 'legal technicalities', inaendelea. Mfano mzuri wa haki kutotendeka ni hukumu ya Halima Mdee na wenzake 18. Kwa kawaida kesi ikiwa inaendelea mahakamani, hairuhusiwi kujadiliwa ili kuepuka kuingilia uhuru wa mahakama. Lakini baada ya hukumu kutoka, ni rukhsa kuijadili kesi husika.

Alhamisi wiki hii, Mahakama Kuu ilitoa uamuzi kuridhia uamuzi wa Kamati Kuu ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuwafuta uanachama wabunge wake 19 wa viti maalum kwa kosa la kughushi kujiteua. Ila Mahakama imewakubalia kwa kupinga uamuzi wa Baraza Kuu, kuridhia uamuzi wa Kamati Kuu, hivyo kikao cha Baraza Kuu kiitishwe upya kusikiliza rufani yao. Jaji Cyprian Mkeha katika uamuzi wake, alisema haki ya asili haikutendeka kwa sababu waliohusika katika kutoa uamuzi Kamati Kuu ndio pia waliokuwa wajumbe katika Baraza Kuu.

Kwa maoni yangu, uamuzi huu wa Mahakama si wa haki hata kidogo kwa sababu msingi wa wabunge hao kufungua shauri mahakamani ni kupinga kufutwa uanachama, kinyume cha katiba, sheria, taratibu na kanuni.

Baada ya kikao cha Baraza Kuu kuridhia uamuzi wa Kamati Kuu ya CHADEMA kuwatimua, ndipo wabunge hao wakakimbilia mahakamani kupinga uamuzi huo.

Mahakama imewapa ushindi CHADEMA kuwa Kamati Kuu imewatimua kina Mdee kihalali na kuwa wabunge hao hawakupinga uamuzi wa Kamati Kuu kuwatimua bali wamefungua kesi kupiga uamuzi wa Baraza Kuu kuridhia uamuzi wa Kamati Kuu kuwatimua, mahakama imebatilisha uamuzi wa Baraza Kuu, hivyo wengi wakaona kina Mdee kama washindi wakati mahakama ni imebariki kutimuliwa kwao.

Nimeisoma hukumu hiyo yote yenye kurasa 79 na kubaini kwamba mosi, Mahakama zetu zinarudia makosa yale yale ya ukosefu wa kutenda haki kwa sababu ya 'legal technicalities'. Mahakama haiwezi kutoa uamuzi wa kitu ambacho hakikuombwa.

Pili, wabunge hawa 19 walivuliwa uanachama wao kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinyume cha haki wa kutokusikilizwa, kinyume cha katiba ya CHADEMA kwa kukiuka sheria, taratibu na kanuni zao wenyewe.

Tatu, Katiba ya CHADEMA inasema mwanachama kabla hajafutwa uanachama, kwanza atatumiwa hati ya mashtaka kwa maandishi kwa 'dispatch', kisha atapewa siku 14 za kujibu mashtaka. Chadema hawakuandaa hati zozote za mashitaka. Hili mahakama ilipaswa ilione.

Nne, baada ya kuitishwa kikao cha Baraza Kuu, kitu cha kwanza kwa Baraza Kuu CHADEMA kuangalia ni uhalali wa kikao cha Kamati Kuu kilichowatimua kina Mdee kama kilikuwa halali na je, Katiba, sheria, taratibu na kanuni za mamlaka ya nidhamu ya CHADEMA zilifuatwa?

Tano, Kamati Kuu ya CHADEMA ni mamlaka halali ya nidhamu ya wabunge wa CHADEMA, lakini si mamlaka ya nidhamu ya Halima Mdee ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA), Mamlaka yake ya nidhamu ni Baraza Kuu, hivyo Kamati Kuu ilipata wapi mamlaka ya kumtimua Mdee? Kikao cha Baraza Kuu kilipaswa hili kuliona.

Sita, japo kikao cha Baraza Kuu kiliitishwa kihalali kama mamlaka ya rufani ya wabunge wa CHADEMA, kitendo cha kikao hicho kubariki uamuzi wa Kamati Kuu kuwatimua bila kufanya mapitio yoyote, ni uthibitisho wa CHADEMA kutowatendea haki wanachama wake.

Saba, kitendo cha Mahakama Kuu kubariki uamuzi wa Kamati Kuu ya CHADEMA, ni mwendelezo wa mahakama zetu kutowatendea haki Watanzania, hivyo kazi ya uelimishaji umma kuhusu Katiba, sheria, haki na wajibu inahitajika sana.

**Paskali.** +255 754 270403

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Watanzania msidanganyike uchaguzi ujao



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

**Hiyo ndiyo Tanzania ambako watu wanafuta vyeo si kusaidia wengine bali kupata chochote cha kunufaika na familia yake, huku mpiga kura akibaki na hali yake ya pangu pakavu tia mchuzi.**

SIKU hazigandi hakika kwa sababu tumebakiza miezi takriban 11 tu hivi tuingie kwenye chekecheke la watu wanaotafuta ulaji mitaani na kama mwaka na miezi 10 kwa wanaosaka kuingia Ikulu na mjengoni.

Hiyo ni miezi ambayo wenye viburi hubadilika na kunyeyekea hata kwa watoto, shikamoo nje nje kama hamnazo, bila kujali hata umri na mvi zao vichwani ili mradi wahakikishiwe wanapata ulaji.

Watanzania anzeni kukaa chonjo, sasa mtafahamika na kila hata ambaye hamjawahi kuonana nao, watajilazimisha kukukumbukeni na hata kukusingizieni kuwa mlisoma wote au mliwahi kukutana jela.

Tayari tumeanza kuona watu wanapitapita vijijini kutimiza ahadi zao walizotoa nyakati kama hizi miaka minne iliyopita kutaka kujionesha kuwa kweli walichoahidi ndicho kinatimizwa leo.

Huku na kule mnasoma na kusikia au kutazama kwenye vyombo vya habari watu wanagawa magari ya kubeba wagonjwa, wengine wanapeleka mabati na mifuko ya saruji shuleni ili mradi ni mihangaiko.

Wale mliokuwa mkiwapigia simu na kujibiwa "simu unayoipigia haipatikani" au "unayempigia anazungumza na simu nyingine", sasa hayo hayapo, ukibipu anapiga na kukuuliza kama una shida.

Hiyo ndiyo Tanzania ambako watu wanafuta vyeo si kusaidia wengine bali kupata chochote cha kunufaika na familia yake, huku mpiga kura akibaki na hali yake ya pangu pakavu tia mchuzi.

Nimesema siku hazigandi, kama walidhani haitafika siku nyingine ya kupanda majukwaani kutudanganya sasa imefika. Madiwani waliotudanganya tukawapa kura wakatupozetea katani, zamu yao ni sasa.

Wabunge waliotufanya mazwazwa kwa kupanda majukwaani kutumwagia miaahadi teletele na kisha kupotelea mijini kuendesha miradi yao binafsi, wajue muda umewadia wa kutoana macho kwenye masanduku.

Wale waomba kura wanyenyekevu na wakipata hujiita waheshimiwa na kuwaona waliowapeleka huko hawastahili heshima, wakiwaeleza kero zao na kuwaita watu wabishi sasa waje tena waone ubishi wao.

Watanzania wenzangu wapiga kura wenzangu, nakushaurini msifanye makosa safari hii mkatuletea kama hawa wanaomaliza muda wao. Tunajua kilichotokea mwaka 2020, kura zetu zilivyozolewa na mafuriko.

Tunakumbuka tulivyochagua tukaporwa haki, baada ya kuambiwa tusichague wale ambao naniliu hakuwa akiwataka akisema ukichagua mpinzani basi sahau maendeleo.

Hakika 2019 na 2020 tuliletewa wawakilishi wala hatukuwachagua, kwa sababu walitakiwa na wachache. ndio walioshinda huku walioshinda wakiachwa bila cha kufanya, kwa sababu ya kuwa na wasimamizi dhaifu.

Mkiona watu wanapigia kelele wakidai Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, msifanye mzaha, watu wamepania na wanamaanisha kweli, kutokana na uzoefu wa huko nyuma, ambako uchaguzi ulichafuliwa na kuwa uchafuzi.

Kama kwetu tutataka kuona haki ikitendeka, basi waacheni watu waunde tume yao ya uchaguzi, ili iwasimamie katika mambo yao ya kupata viongozi, ili hatimaye tusijelaumiana kuwa na Taifa la songombingo.

Na kama kweli nchi hii ni yetu sote kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan husema na hata kuonesha, basi hili halihitaji mvutano na kutoana macho kulifanya ili uchaguzi ujao uwe wa mfano duniani.

Lakini kama tunaona ni porojo tu za Watanzaia waliozoea kila kitu kumwachia Mungu, basi tujiandae kuona nusu ya waliojiandikisha hawajitokezi kupiga kura, kwa sababu watakuwa hawaoni umuhimu wake.

Jiulizeni mathalan, nani atajitokeza kupanga mstari kupoteza muda wake huku anaumwa njaa, hana chakula na kilichopo bei yake haishikiki? Nani atajipanga kuchagua na mwishowe aletewe asiyetakiwa?

Hivi nani kwa kweli atakubali kuwa na Bunge kama hili linalomaliza muda wake? Bunge la 'chama kimoja' la kupitisha kila kinachopelekwa, huku nje wahusika wakisema tofauti na wanachokifanya mjengoni?

Kama vipi tusikubaliane kuja na sheria za kuruhusu wagombea binafsi, ili tusitegemee kupata wawakilishi walio kwenye vyama, hata kama hawana sifa ila sifa ni uanachama wa chama cha siasa? Tusipoteze muda wa Watanzania kupiga kura na kuvuna mabua.

Mimi ngoja nitangaze mapema tu kwamba mambo yakienda sawa na tukakubaliana wagombea binafsi, basi kama si Tanzania, Segerea itanihusu kwa maana ya kuongoza nchi au jimbo mtawalia. Mpo? Ni haki yangu atii! Watanzania amkeni, nchi hii ni yetu sote!

**Mungu na atubariki!**

## Vyakula vya stendi, barabarani vyaweka hatarini afya za walaji

INATOKA UK. 4

maalum vya kubebea vyakula.

Wauzaji hao hawakuwa na sare huku baadhi yao wakiweka vikapu vyao chini walipopakua chakula kwa ajili ya wateja wao. Pia hawana vifaa vya kuvaa mikononi, wakipakua chakula kwenye sahani za plastiki na wengine kwenye mifuko plastiki.

**MAMLAKA ZINASEMAJE?**

Ofisa Afya Mkoa wa Kilimanjaro, Happynus Pilula, anaanza kwa kutaja matakwa ya kisheria katika uanzishaji biashara ya chakula.

Anarejea Sheria ya Afya ya Jamii (2009) kifungu cha 32 inayoelekeza kwamba ili mfanyabiashara afungue eneo la biashara ya chakula, lazima awe na eneo la kuhifadhia chakula ambalo lina ukubwa wa kutosha, lisitunze unyevu, liwe na mwanga wa kutosha, lenye kupitisha hewa, liwe safi na lisiwe na wadudu vamizi, lisiwe karibu na choo, liwe na sakafu, kuta na dari zinazosafishika.

Pilula anasema wakati wa utoaji huduma watoahuduma wanapaswa kuvaa sare safi na viatu vya kufunika, wanawe mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka, wafanyiwe uchunguzi wa kiafya mara moja kila baada ya miezi sita na wanapaswa kutoa taarifa haraka ya kiashiria cha ugonjwa wowote unaoambukizwa kwa chakula.

"Mtoahuduma hapaswi kushika chakula ikiwa ana ugonjwa wowote wa ngozi hususani katika mikono, hasa ikiwa hilo eneo haliwezi kufunikika, asiteme mate, kutoa kamasi, asipige chafya, asivute sigara wala kutafuna chochote wakati wa kuandaa chakula au kuhudumia.

"Hapaswi kuvaa pete kidoleni, hapaswi kuvaa ndala, hapaswi kuwa na kucha ndefu wala zilizopakwa rangi na hina, hapaswi kuweka rangi kwenye nywele, lazima awe amefunika kichwa.

"Masharti haya yanakwenda sambamba na ukaguzi wa jengo ambao hufanywa na TBS (Shirika la Viwango Tanzania) na leseni ya biashara kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)," anafafanua.

Ofisa Afya Pilula anasema uuzaji holela wa chakula ni jambo lisilokubalika kisheria. Kutokana na dosari zilizobainika katika Stendi Kuu ya Moshi na maeneo jirani, watakaa na wataalamu wa mkoa wake ili kutatua changamoto hiyo.

TBS katika ufafanuzi wa Novemba 14, mwaka huu, kupitia kupitia kwa Meneja Uhusiano na Masoko, Gladness Kaseka, ilisema Sheria ya Viwango, Sura 130 na kanuni zake, imepewa jukumu la kusimamia usalama wa chakula na ubora wa bidhaa za chakula na vipodozi kwa lengo la kulinda afya ya jamii.

"Maeneo ya biashara yanayohitajika kusajiliwa ni pamoja na hoteli za kitalii, na za kawaida, supermarkets (maduka makubwa ya bidhaa mbalimbali), maduka ya jumla na rejareja ya vyakula na vipodozi.

"Mashine za kuchakata nafaka na mazao mengine yasiyofunganishwa, wauzaji na wasambazaji wa chakula kwenye mikusanyiko, vioski, baa na maghala ya vyakula na vipodozi, migahawa na magari yanayobeba vyakula na vipodozi," anasema Kaseka.

Alitoa tahadharisha kwa wafanyabiashara wote kuwa atakayekutwa anauza, kuhifadhi au kusambaza bidhaa za chakula na vipodozi bila kusajili jengo lake, atachukuliwa hatua za kisheria.

ITAENDELEA KESHO

# Mifumo kuwabana watumishi goigoi

**Na Lusungu Helela,**
ARUSHA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amesema matumizi ya mifumo wa PIPIMS, PEPMIS na HR Assessment itaimarisha utumishi wa umma kwa kuwabana watumishi wanaopenda kukaa ofisini pasipo kufanya kazi.

Kikwete alisema hayo jana jijini hapa wakati akizungumza kwa nyakati tofauti na watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha ( AICC) na Chuo cha Ufundi Arusha.

Vikao hivyo na watumishi hao ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi ya kukagua mafunzo ya matumizi ya mfumo wa kupima utendaji kazi wa watumishi wa umma na taasisi (PEPMIS na PIPMIS) na Mfumo Maalum wa Tathmini ya Hali ya Rasilimali Watu Serikalini (HR Assessment).


Alisema serikali imedhamiria kuimarisha utumishi wa umma kwa kuhimiza uwajibikaji ili kuhakikisha taifa linakuwa na utumishi wa umma unaopimika kwa kumpima mtumishi mmoja mmoja pamoja na taasisi kwa ujumla.

Aliongeza kuwa PEPMIS imekuja kuwa mbadala wa OPRAS ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan anayelenga kuimarisha mifumo ya uwajibikaji inayowezesha viongozi na watumishi wa umma kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi wakati na mahali popote.

Katika hatua nyingine, Kikwete aliwataka maafisa utumishi na maofisa tawala kuacha kukaa ofisini badala yake waende maeneo ya kazi ili kusikiliza changamoto zinazowakabili watumishi walio chini yao.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, alisma zama hizi hazihitaji watu wenye misuli kutokana na kukua kwa teknolojia, hivyo teknolojia imerahisisha utendaji kazi na sisi tuko tayari kuisimamia utekelezaji wake.

Alisema ujio wa mafunzo hayo umekuja wakati mwafaka kwa kuwa maofisa utumishi na maofisa tawala wataanza kubadilika na kuachana na utaratibu wa kizamani wa utendaji kazi wao. Mongela alitumia fursa hiyo kuiomba Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora kuwanoa upya maofisa utumishi na maofisa utawala wa mikoa na halmashauri kwa kuwa utendaji wao wa kazi si wa kuridhisha ikizingatiwa wao ndio wenye jukumu la kuwasimamia watumishi wengine.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, akiwa na Mkuu wa Chuo cha Arusha (ATC), Dk. Musa Chacha, wakiangalia baadhi ya mashine za kufundishia wanafunzi kwa vitendo katika chuo hicho jana. **PICHA: LUSUNGU HELELA**

# Watu 600 wapata mafunzo uhudumu wa ndege

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Mafunzo ya Wahudumu wa Ndege cha ATTC, kimetoa mafunzo ya kitaalamu kwa wahudumu 600 tangu kianzishwe miaka 10 iliyopita.

Mkuu wa Chuo hicho, Elly Ndekile, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza kwenye mahafali ya chuo hicho ambapo wahitimu 72 walitunukiwa vyeti vyao.

Alisema kutokana na ubora wa wahitimu wa kituo hicho na kozi wanazotoa, kampuni mbalimbali za ndani na nje ya nchi zimekuwa zikichukua wahitimu hao na kuwaajiri kwenye kampuni hizo.

Ndekile alisema tasnia ya usafiri wa anga inazidi kukua kutokana na kampuni za usafiri wa anga kuendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka na idadi ya safari za ndege nazo zikizidi kuongezeka hali ambayo inaongeza nafasi za ajira za wahitimu wa chuo hicho.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa wahitimu wa chuo hicho wamekuwa wakifaulu mitihani wanayopewa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) na kupatiwa leseni ya kufanyakazi ndani ya ndege.

Kadhalika, Mkuu huyo wa chuo alisema wanakabiliwa na changamoto ya uhaba wa madarasa hali ambayo inawafanya washindwe kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi wanaoomba kupata mafunzo kwenye chuo hicho.

Alisema pamoja na changamoto hiyo uongozi umejipanga kuhakikisha wanatumia rasilimali zilizopo kufikia mahitaji ya makundi na kuongeza idadi ya kozi zinazotolewa chuoni hapo.

"Chuo kitaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali na tunatarajia kuongeza idadi ya kozi kwa kadri mahitaji yanavyokua na kwa sasa kozi tano zitaongezeka kabla ya Juni mwakani na mwaka 2025 tutaongeza kozi kumi," alisema.

Alisema ATTC ni kitengo kilichoanzishwa ndani ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ambacho kilianzishwa kwa lengo la kuwapa mafunzo wafanyakazi wa shirika hilo na wasio wafanyakazi wa shirika hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi, alisema shirika hilo lilianzisha chuo hicho kwa ajili ya mafunzo kwa wafanyakazi wake pekee lakini kutokana na mahitaji kuongezeka waliamua kufungua fursa kwa wasio wafanyakazi kusoma.

Aliupongeza uongozi wa chuo hicho kwa namna ambavyo umefanikiwa kutekeleza maono yake na kufanikiwa kutoa idadi kubwa ya wahitimu wanaofanyakazi nchini na kwenye mashirika mengine duniani.

Alisema menejimenti ya ATCL inakiangalia chuo hicho kwa jicho la kipekee kutokana na umuhimu wake kwenye ustawi wa shirika hilo.

Alisema maboresho yanayoendelea ndani ya shirika yalianza mwaka 2016 wakiwa na wahudumu 30 lakini kwa sasa shirika lina wahudumu 165.

"Kwa takwimu hizi unaweza kuona umuhimu wa chuo hiki na namna kilivyotuwezesha kupata wahudumu ndani ya ndege, wakati tunaanza maboresho ya ATCL mwaka 2016 tulikuwa na kituo kimoja nje ya nchi na vituo vinne ndani ya nchi lakini kwa sasa tunavyo vituo 15 ndani ya nchi na 10 nje ya nchi jumla vinafikia vituo 25," alisema Matindi

"Haya nawaambia ili mjue kwamba hamkupoteza fedha zenu kusomea kozi hii, Air Tanzania inaendelea kukua na kuhitaji wahudumu wa ndani ya ndege waliopata mafunzo bora," alisema.

# MAISHA

DESEMBA 17, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*

Ukurasa 14




## Saladi ya mboga

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



Ifanye nyumba iwe nyumbani, kila mtu afurahie sikukuu za mwisho wa mwaka




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# HINA UREMBO WA KALE

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| N | ■ | U | H | U | R | U |
| Y | ■ | ■ | ■ | M | ■ | S |
| E | ■ | L | O | A | ■ | H |
| R | A | I | ■ | N | I | A |
| E | ■ | S | A | A | ■ | M |
| R | ■ | H | ■ | ■ | ■ | B |
| E | L | E | W | A | ■ | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

GUU, MBU, MBA, TEE, SHULE, ASALI, GAMBA, UBUTU, ELIMIKA, ENDESHA

## AMSHA AKILI





## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

BAADA YA JAMBAZI KUVAMIA KANISA

Jambazi mmoja aliingia kanisani na bunduki akapiga risasi juu ya bati akasema “asiyempenda YESU atoke nje” wakatoka wote isipokuwa mchungaji na wazee wawili.

Jambazi likamwambia mchungaji “unaweza kuendelea na ibada, nilikuwa nakuondolea wanafiki”, Mchungaji akasema “ungewaacha kwanza nichukue sadaka...!

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Jaribio kuua ndoa ya mwenzako linapofeli

MPENZI msomaji, karibu tuendelee na vituko vya safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Dada mmoja alikuwa na sherehe ya mahafali ya mdogo wake mkoani Kilimanjaro hivi karibuni.

Akaambatana na mama mzazi na ndugu wengine kwenda kwenye sherehe. Kule Moshi alikuwa na mama rafiki wa siku nyingi ameolewa anaishi na mumewe na watoto. Huwa wanatembeleana.

Wakati dada huyu akisafiri kwenda Moshi kwenye mahafali hiyo, mumewe alikuwa safarini mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kikazi, hivyo hakushiriki sherehe hiyo. Maandalizi ya shughuli yalikuwa mazuri kule walikofikia kwa wenyeji na sherehe ilifana sana. Walichangamka na walishapanga kufanya wote biashara na mama mwenyeji wake, huku mumewe akiahidi kumpa mtaji wa kuanzia.

Lakini siku moja kabla ya hawa wa Dar kurejea, likatokea vagi la mwaka nusura ndoa ya wenyeji wake ivunjike kama si mkono wa Mungu ulisimama na kutenda haki.

Kilichotokea ni kwamba mumewe bibie wa Dar alimpigia simu mkewe na kumwuliza huko Moshi wamefikia hoteli gani. Bibie akamjibu kuwa hawakufikia hotelini bali nyumbani kwa mama fulani ambaye hata yeye (mumewe) anamfahamu.

Bwana huyu wa Dar akang'ang'ana anataka mawasiliano na baba mwenye nyumba hiyo athibitishe kama kweli mama mkwe na mkewe wamefikia nyumbani hapo. Kupewa namba ndio balaa likaanzia hapo!

Yule jamaa wa Dar akaanza kummwagia upupu baba mwenyeji kule Moshi eti mkewe ni mhuni asingemruhusu afikie nyumbani kwake kwani atamharibu kitabia mkewe.

Baba wa Moshi baada ya mazungumzo ya simu aliporejea jioni alibadilika na kuwasalimu wageni bila uchangamfu. Aliingia chumbani na kumuita mkewe. Akamweleza yote aliyoambiwa na jamaa wa Dar kuhusu tabia ya mkewe na kwamba asipokuwa makini atamharibu pia na yeye.

Mama yule wa Moshi hakuruhusiwa tena kutoka chumbani. Hali hii iliwashangaza sana wageni yaani bibie na mama yake.

Kulipokucha, siku ambayo wageni hao walikuwa wanaondoka, mama mwenyeji aliandaa kifungua kinywa. Wakajiandaa kuondoka lakini kabla mama na bintiye waliomba kufanya sala ya kuagana. Maombi yale yaliongozwa na mama mgeni ambaye aliomba wote wasimame washikane mikono wakati akiomba.

Baada ya maombi hayo ya upatanisho, kuzuia maneno ya uchochezi badala ya kuimarisha upendo na amani, wote waliagana na kuondoka. Mama huyu anasema wakati wote akiwa safarini bado alikuwa kwenye maombi akiomba Mungu aepushe shari na kuvunja nguvu zote za giza zinazojaribu kuvunja ndoa takatifu.

Baada ya kureja Dar, mama mwenyeji wa Moshi aliwapigia simu akitaka kujua kama wamefika salama. Pia aliwaambia kuwa baada ya kurudi nyumbani mumewe alimwita chumbani na kujadiliana kile kilichotokea na kumuomba msamaha.

Inavyoonekana mumewe alijilaumu kuchukulia mazungumzo yale ya simu na mwanamume mwenzie kwa jazba bila kutafiti kwanini jamaa huyo wa Dar amweleze tabia zisizofaa za mke wake na kwamba nisimwambie. Ebo! Tuhuma hizo asimwambie?

Mama wa binti waliporejea Dar, alimwendea mkwe (mume wa mwanawe) kumuuliza kwa nini alitaka kuvunja ndoa ya wenyeji wao kule Moshi kwa kueleza vitu vya uongo dhidi ya mkewe na kwamba eti mume wa Moshi amuonye mkewe asiwe na mawasiliano na mama watoto wake kwani atamharibu kitabia?

Bila aibu na bila kuamini kuwa mambo yote ni hadharani akakana kupiga simu. Baada ya kusutwa, jamaa alimpigia simu baba wa Moshi akimuuliza kwa hasira eti ni kwa nini alimweleza mkewe juu ya mazungumzo yao ya simu.

Mpenzi msomaji, Hivi utapewa tahadhari mkeo kumuepuka mtu fulani kisa atamharibu kitabia nawe ukae kimya usimwambie? Hatua hii ndiyo iliyozidi kumpa viashiria jamaa kwamba baba yule wa Dar ni mzushi, mvunja ndoa za watu, huku akimharibia mkewe kwa maneno ya uwongo ili akose marafiki.


Hata hivyo, jamaa wa Moshi amempuuzia na sasa mahusiano na mkewe yamerejea kama kawaida na amesema ataendelea kumruhusu mkewe afanye biashara na bibie aliyefikia kwake kwani mume wake anaonekana na matatizo kichwani mwake.

Mkono wa Mungu ukiingilia kati hakuna linaloshindikana. Maombi ya wageni yalisimamia haki. Nyumba zingine ibilisi hana nafasi nguvu za Mungu zimesiliba pande zote.

**Je, una maoni, kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Umeyaweka maisha rehani, mitandao inakuzuzua

UKIONA umeanza kupoteza matumaini, ujue uko njiani kupoteza sababu za kuishi. Kama hujui, katika maisha poteza vyote ila usipoteze matumaini.

Ni dhahiri shahiri kwamba hasira ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu katika hili, usinidanganye!

Umeamua kukufuru, umejipa jukumu la kuwa askari kanzu wa maisha ya wengine na umesahau maisha yako. Walichokufanya, ndiyo maana unaona umepoteza matumaini ya kuishi.

Haya yote yanatokana na kuperuzi maisha ya watu. Umebeba vinyongo na visasi moyoni vinavyokufanya uwafikirie waliokuumiza zaidi kuliko kufikiria furaha na maendeleo yako.

Ndugu yangu, hauwezi kufanikiwa kwa sababu hujui tu, una mizigo mingi isiyo ya lazima, wala faida ambayo umeibeba.

Kucha, kutwa! uko mitandaoni. Kwa kifupi, huna siri. Unatamani mafanikio tu moyoni, lakini huna mipango ya kuyafikia.

Kila aliyefanikiwa ni rafiki yako, aisee hivi hujifunzi kutokana na mafanikio yao?

Kwa nini hutamani kutumia fursa hiyo ya kujuana nao na kujifunza ili na wewe upate mafanikio, na siyo kujikatia tamaa?

Ndugu yangu elewa kwamba haya maisha si mashindano na watu wengine. Mashindano uliyo nayo na unayotakiwa kushindana nayo, ni kuhakikisha kila iitwapo leo, unapata kitu kipya cha kukufanya uzidi kuwa bora zaidi.

Laiti ungelijua kwamba uliumbwa kwa kusudi maalumu na ulipewa uwezo wa kuwa vile unatakiwa kuwa, usingekata tamaa na kupoteza maana ya kuishi.

Wengi wetu hatujui ukweli huu kwa kuwa hatukupata watu wa kutuambia au kutuongoza, lakini shukuru Mungu umesikia hili sasa kama hukujua.

Ni wajibu wako wewe kuishi na kutembea katika ufahamu mpya ulioupata kuhusu wewe ili uweze kuwa bora zaidi.

Hebu ndugu yangu amua kwa dhati kwamba badala ya kupoteza muda kufanya yasiyokuhusu, yasiyokuwa na tija kwako, basi amua kufanya ya maana.

Jitafute tena, badala ya kukata tamaa na kuanza kupoteza maana halisi ya kuishi na kufanikiwa.

Wenye akili, hutamani kukimbia mbio zao wenyewe lakini wewe unataka kushindana na fulani. Ukikwama kinachofuata ni hasira, kughairi na kukinai mafanikio.

> **Umeamua kukufuru, umejipa jukumu la kuwa askari kanzu wa maisha ya wengine na umesahau maisha yako. Walichokufanya, ndiyo maana unaona umepoteza matumaini ya kuishi.**

Hakuna namna nyingine ya kukwepa mtego huu zaidi ya kuingia kwenye mashindano na wewe.

Jitahidi sana kuwa bora zaidi ya jana. Hebu jichunguze uone namna ulivyo wa dhahabu. Kila mtu ana nafasi ya kung'ara kwenye eneo lake.

Hakuna nyota inayozuia nyota nyingine kuonekana angani ila usisahau kuwa kila nyota huwa inatofautiana nguvu ya kung'ara kwake.

Badala ya kuhangaika kuzuia nyota nyingine kung'ara, weka bidii kuongeza mng'aro kwenye nyota ya kwako.

**• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI







Katika harusi watu wengi wanavutiwa na gauni la bi harusi na wapambe wake, hivyo gauni la hariri rangi ya bluu linavutia zaidi wakati wa kufunga ndoa.

# MITINDO








# RAHA KUVAA JEZI

HIVI karibuni kumekuwa na kawaida ya watu kuvaa jezi za timu za soka wakati wanapokuwa matembezini au katika maeneo yao ya kazi.

Vazi hili ambalo linatumika kama sare za wacheza soka wakati wakitumikia timu zao, limezidi kuwapagawisha mashabiki zao na kulifanya kama rasmi katika shughuli zao za kawaida.

Je kwa nini watu wengi wamegeukia kuvaa jezi za timu za soka kuliko ilivyokuwa huko nyuma?

Haya ndio majibu ya baadhi ya wadau mbalimbali wa mavazi walivyosema.

"Jezi ni nguo rahisi kununua, kuzitunza na zinaendana na kipindi kirefu cha joto kwa nchi za Kiafrika," amesema Yoranda John.

Juma Mnata amesema " Jezi hazihitaji pasi kuzinyoosha, ukifua inawahi kukauka, inavalika usiku na mchana bila shida,"

"Unaweza kupata rafiki sehemu yoyote na kuondoa upweke na hata kama umepotea ni rahisi kupata mtu wa kukuelekeza." Ameongeza.

Aisha Kashinde kwa upande wake amesema "Jezi huwa haichafuki haraka, uchafu unatoka haraka wakati wa kufua na inampendezesha mtu pale anapovaa,"

Kareem Abdallah ameeleza kwamba jezi huwa haichagui nguo ya kuvalia chini kwani inapendeza kwa jinzi, pensi, suruali kitambaa, kadeti na hata msuli.

"Unaweza kuvaa jezi na ukaenda msibani, club, baa, ufukweni hata ofisini bila tabu kwa sababu hazichoshi machoni.

UREMBO

Na Mary Geofrey



# HINA UREMBO WA KALE unaofurahisha vijana

RANGI inayotokana na mti wa hina ni urembo wa kale unaoendelea kutumika hadi sasa.

Majani ya hina ambayo yanatoa rangi ya njano iliyokolea yametumika kwa miaka mingi kwa wanawake na wanaume kwa ajili ya urembo wa kujipaka mwilini na katika nywele au ndevu.

Hina hupatikana kupitia majani makavu yaliyosagwa na mara nyingi hupatikana nchi za Afrika Kaskazini na Asia Kusini.

Rangi hii inakuruhusu kuchora juu ya ngozi au kupaka kwenye nywele bila kupata madhara.

**Faida za hina**


Hina mbali na kubadili rangi ya nywele, inalinda ngozi ya kichwa kwa kuongeza maji na kupunguza mba na muwasho kichwani.

Husaidia kuimarisha nywele zako bila kukamaa au kukatika na kuendelea kuwa na mvuto.

Kama tulivyosema hapo awali, ikiwa hina tunayotumia ni ya asili kwa asilimia 100, haina athari zozote kwa mtumiaji.

Rangi hii inaweza kutumika kwa kila aina ya nywele, au ngozi na inatoa matokeo bora katika nywele za asili.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Saladi ya mboga



SALADI ni aina ya kachumbari inayoungwa na viungo mbalimbali kwa ajili ya kula na vyakula mbalimbali.

Wengi tumezoea kutengeneza kachumbari za kawaida za kuchanganya nyanya, kitunguu, tango na limao, lakini saladi ni tofauti kidogo.

Leo kwenye safu ya mapishi tutaelezana namna ya kutengeneza saladi ya mboga ambayo ni rahisi na haitumii muda mrefu.

**Mahitaji**

Viazi saba vya ukubwa wa kawaida, maharage machanga ya kijani kikombe kimoja, karoti moja, mahindi kikombe kimoja, njegere kikombe kimoja, mayonnaise vijiko vitatu vya supu na kitunguu saumu chembe tatu.

Mahitaji mengine ni chumvi kiasi, pilipili manga nusu kijiko cha chai.

Namna ya kutayarisha na kupika

Chemsha viazi kiasi visiive sana hadi kuvurugika. Kisha menya na kata vipande vidogovidogo, weka kando.

Menya na kata karoti vipande vidogovidogo weka kando. Chemsha maharage machanga, mahindi na njegere. Yakiwa karibu na kuwiva tia karoti na maji kiasi ya kuchemshia.

Katika bakuli la kupakulia saladi, weka viazi na karoti na njegere, maharage na mahindi uliyoyachemsha.

Chuna au saga kitunguu thaumu, changanya vizuri na mayonnaise, chumvi na pilipili manga.

Kisha mimina katika bakuli pamoja na mchanganyiko wa viazi na mboga, maharage, na saladi yako itakuwa tayari.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Ifanye nyumba iwe nyumbani, kila mtu afurahie sikukuu za mwisho wa mwaka

MIONGONI mwa maeneo ambayo huwa ni faraja na ya kupumzisha akili baada ya shughuli nyingi ni nyumbani.

Nyumbani ndipo palipo na mkusanyiko wa maisha, kumbukumbu na upendo kwa asilimia kubwa ya watu.

Binadamu kila mmoja hujishughulisha na mambo mbalimbali lengo likiwa ni kujitafutia riziki na kuhakikisha mkono unakwenda kinywani na mambo mengine ya kifamilia yanakwenda sawa.

Lakini pamoja na kujishughulisha huko, mwisho wa siku lazima arejee nyumbani kujipumzisha bila kujali umbali wake, hivyo kwa vyovyote vile lazima uhakikishe nyumbani kunakuwa mahali sahihi, panapokupa furaha na panafanyika kuwa nyumbani kweli kweli.

Na katika kipindi kama hiki cha mwisho wa mwaka, wengi hupenda kuchukua mapumziko ya kikazi, kwa hiyo ili kutengeneza mwanzo mzuri wa shughuli za kila mwanafamilia kwa mwaka unaofuata ni muhimu kuhakikisha nyumbani panafanyika pa faraja, amani na furaha.

Si tu kwa utulivu, lakini panawekwa vizuri kimazingira na kuwapo na madhari ya kuvutia mtu kupumzika. Ziko njia mbalimbali za kufanya ambazo hazihitaji gharama kubwa ya kifedha ambazo ni rahisi na ni vitu vidogovidogo.

Mojawapo ni mapambo, ndani ya nyumba yako unaweza kutafuta baadhi ya picha za mapambo ambayo unayapenda na ukapamba.

Tumia pia picha nzuri ziwe za kuchora au zinazoonyesha alama ya upendo au yoyote inayokukumbusha enzi au nyakati fulani.

Ipe nyumba yako mwonekano na hisia inayotambulisha familia au aina ya watu wanaoishi katika nyumba husika au familia uliyowahi kuwa nayo awali.

Hakikisha mwonekano wa nyumba usiwe unaofanana siku zote hususani ndani kuanzia sebuleni, vyumba vya kulala na hata nje kwenye mpangilio wa maua kwa wale wenye nafasi kubwa.

Kila nyumba ina upekee wake na mahitaji tofauti kuendana na wakaaji wake.

Pia usafi ni jambo jingine la kuzingatia ambalo linapaswa kuzingatiwa katika kuweka mazingira yake kuwa ya kuvutia kukaa wakati wote.

Bila kusahau suala la mapishi, ili nyumbani au mtu ajisikie yuko nyumbani lazima kuwe kunapikwa chakula.

Kuna baadhi ya nyumba ambazo hakupikwi, ni watu wa kula barabarani tu. Ili nyumba yoyote ile igeuke kuwa nyumba ni muhimu sana kuwe na chakula, yaani jiko linapotumika kuandaa vyakula na harufu yake nzuri inaifanya kuwa na uhai wa kuitwa nyumbani.

Hata wanaoishi katika nyumba hiyo lazima wajisikie fahali kuishi humo na pia kukumbuka na kupenda kuwapo nyumbani muda wote.

## DONDOO

### Fahamu matumizi ya 'boga' kwenye mapambo

**Na Restuta James**

SUALA la kupamba nyumba au eneo lolote ni sanaa ya ubunifu inayoleta ladha nzuri na kuonesha hisia za mpambaji.

Wataalamu wa mapambo wanaeleza kuwa unaweza kuelewa mawazo na hisia za mpambaji kupitia sanaa hii.

Mbunifu wa mapambo ya ndani, Jenna Kate, anazungumzia upambaji wa makabati ya vitabu majumbani akieleza kuwa vitabu vikipangiliwa vizuri vinaweza kuleta mwonekano wa pambo.

Anasema si vyema vitabu vikakaa vyenyewe kwenye kabati bali ili panoge panahitaji mchanganyiko wa nakshi za zamani na za kisasa yakiwamo 'maboga'.

"Kwa kuwa vitabu havipitwi na wakati, unaweza kuweka vichache vya zamani na vipya, picha yako ya utoto au yazamani ya familia...ukitumia mbinu na vidokezo hivi utatengeneza mazingira yenye mchanganyiko wa hisia, jambo ambalo ni zuri sana," anasema.

Jenna anasema ili kunogesha mwonekano, ongeza pambo la boga katika kila shelvu ukiweka la rangi nyeupe, dhahabu na njano ili kuweka mwonekano wa 'uzamani' na usasa.

**DONDOO MUHIMU**

Tanguliza picha kubwa juu ambayo inaweza kuwa ya kuchora au ya familia.

Weka vitabu vidogo pamoja kwa makundi yake na usiweke vingi sana. Staili hii itumike pia kwenye kupanga maboga yako, unaweza kuweka kubwa na dogo kwenye eneo moja.

Hakikisha kuna nafasi ya wazi inabakia kwenye kabati lako, mpangilio ni pamoja na kuwa na 'open space.' Hii itasaidia kuruhusu mzunguko wa hewa.


Kabati la vitabu au vyombo halipaswi kuwa na vitu hivyo pekee, linahitaji nakshi za kulifanya livitie zaidi. Inashauriwa 'kutupia' picha yenye madhari nzuri na itapendeza ikiwa ni ya safarini au yenye wanafamilia wengi.

Badili mwonekano kulingana na majira. Unaweza kuweka maua fresh katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka au mapambo ya Krismasi kwa Wakristo.



Usisahau kuweka jagi lenye maua makavu yenye rangi uipendayo. Katika eneo hili, zingatia sana urefu wa 'vase' yako kulingana na mpangilio wa vitu vingine.

## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
SIKUKUU ZA MWISHO WA MWAKA ZINAKUTIAGA WAZIMU SAFARI HII UTAZIONEA HAPO!
NAKUAHIDI UKINIRUHUSU NITAHAKIKISHA HATA NILEWE VIPI HUKUTI 'MIZIGO' KWENYE SURUALI
X-MASI OYE!
KAKA NAONA NI MWENDO WA MIKEKA TU, MPAKA WATANYOOKA KULALEK!
WENYEWE UTAWASIKIA 'AFWANDE USINI-BETIE NAKUFINYIA NY@MB#F!'
ONGEZEKO LAKO LA NAULI NDIO TAMKO LA SEREKALI AU HALIMASHA-URI YA BICHWA LAKO?
WEWE USINIAMBIE MIMI BICHWA LANGU NITAKUTIMBATIMBA! NAULIZA UTATOA UTOI?
MTIMBE UONE KAMA UJAZOLEWA NA CHEPE NA SITE! UMBWA WE!
HUYU KONDA MWILI WAKE UNAMUWASHA ANAHAMU YA VIDONDA ARINGISHIE MWAKA MPYA
KUMBE UJAKAA SANA JELA KAMA TULIVYOFIKIRIA!
MLIFIKIRIA NITAKAA SANA KUMBE MWENZENU NILISIMAMA SANA'
NINACHOJUA MIMI KICHWA CHA NYOKA HAKIBEBI MZIGO
'DOMO KA'BATA!'
NACHOJUA MIMI DEBE TUPU HALIACHI KUPIGA MIKELELE MZOEA VYAKUNYONGA VYAKUCHINJA HAVIWEZI
'BONGE MZITO'
WEWE KAA USUBIRI SIKUKUU ZIFIKE UFAKAMIE PILAU... USINICHUNGUZE
NAULIZA TU SAFARI HII 'UBECHE' HAPA HAPA AU UTABETI NYUMBA GANI TUTAALIKWA?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
OLEWA UWATAMBIE HAWARA ZAKO WA ZAMANI...

## HABARI KIMATAIFA

# Jeshi la Israel laua mateka watatu

**TEL AVIV,** ISRAEL

JESHI la Israel limetangaza kuwaua kimakosa mateka watatu wakati lilipofanyika shambulizi la risasi jana Ukanda wa Gaza.

Watu hao walitambuliwa kwa majina Yotam Haim (28), Samer Talalka (22) na Alon Shamriz (26) walilengwa katika shambulizi hilo baada ya kutambuliwa kama wanamgambo wa Hamas.

Hata hivyo, jeshi hilo lilielezea majuto yake na kusema watatu hao walipigwa risasi na wanajeshi wanaoendesha harakati za kijeshi katika eneo la Shejaiya, kaskazini mwa Gaza.

Zaidi ya raia 100 wa Israel wameendelea kuwa mateka na kuhifadhiwa miji mbalimbali ya Gaza baada ya kukamatwa katika mashambulizi ya Oktoba 7 yaliyofanywa na hamas nchini Israel.



Kutoka kushoto kwenda kulia ni Alon Shamriz, Yotam Haim na Samer Talalka.

Jeshi hilo lilisema tukio hilo linachunguzwa, na kwamba ni kitendo cha kujutia na kusikitisha na linatuma rambirambi kwa familia zao. "Dhamira yetu ya kitaifa ni kutafuta waliopotea na kuwarudisha mateka wote nyumbani," liliongeza taarifa hiyo.

Baada ya taarifa hiyo mamia ya watu waliandamana katikati mwa mji mkuu wa Tel Aviv kushinikiza serikali kuhakikisha inafikia makubaliano ya kuwaachilia mateka waliosalia.

Waandamanaji walishika mishumaa na kubeba mabango yaliyoandikwa "Walete nyumbani" na "Kubadilishana mateka sasa!"

Miili ya watu hao watatu ilirudishwa katika ardhi ya Israel, ambapo ulipofanyika ukaguzi ulithibitisha utambulisho wao.

**Wakati huo huo,** Ikulu ya Marekani ya White House ilielezea mauaji hayo ya mateka watatu wa Israeli ni sawa na kufanya kosa la kutisha.

Msemaji wa Baraza la Usalama la taifa, John Kirby, alisema Rais Joe Biden alikuwa amefahamishwa kuhusu tukio hilo.

Msemaji huyo alieleza imani yake kwamba Waisraeli wanatambua jinsi gani ya kufanya ili kosa kama hilo lisifanyike.

Alisema jeshi la Israel lilielezea masikitiko yake kutokana na mauaji ya wafungwa hao yaliyofanywa kwa bahati mbaya.

Israeli inaamini kuwa kitongoji hicho ni ngome ya kufanyia harakati za mapambano ya kundi la Hamas, na ni kitovu cha mapigano kwa siku kadhaa.

**BBC**



Kikosi cha Jeshi la Israel kikirusha makombora kutoka kwenye kifaru kuelekea Ukanda wa Gaza juzi. **PICHA: AP**

# Wagombea DRC washambuliwa mitandaoni

**KINSHASA,** DRC

IKIWA zimebaki siku tatu kufanyika kwa uchaguzi mkuu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, wagombea wa nafasi za urais wamelalamika kufanyiwa mashambulizi ya kimtandao.

Wagombea hao wamedai kwamba zinasambazwa taarifa za uongo kwenye mitandaoni kwa nia ya kuharibu sifa za wapinzani wanaoshiriki kinyang'anyiro cha urais.

Madai hayo ni pamoja na kuwepo wagombea feki au kuwataja baadhi ya wagombea kuwa ni raia wa kigeni. Madai hayo yanadaiwa kutumiwa kama silaha kwa ajili ya kuwamaliza kisiasa baadhi ya wagombea wa upinzani.

Mwandishi wa habari wa tovuti inayochunguza ukweli kuhusu Congo (Kongo Check), Marien Nzikou-Massala alichapisha jumbe zinazolalamikiwa kuwa kuna baadhi ya wagombea ni wazambia, wagiriki na zingine zikienda mbali na kueleza kuwa mgombea ameoa mwanamke mwenye asili ya Rwanda. Mwandishi huyo aliongeza kusema, katika kipindi cha uchaguzi mjini Kinshasa, taarifa potofu zinaenea kwa kasi zaidi kuliko taarifa sahihi. Tangu kuanza kwa kampeni ya uchaguzi wa Desemba 20, mashambulizi ya mtandaoni yamekuwa yanawalenga zaidi wapinzani wanaoaminika kuwa ni tishio zaidi kwa Rais Felix Tshisekedi, ambaye anawania muhula wa pili.

Mashambulizi hayo yanawalenga wagombea wa upinzani akiwemo mfanyabiashara tajiri, Moise Katumbi na mshindi wa tuzo ya amani ya Nobel Denis Mukwege, kuwa ni wageni waliopewa uraia wa Congo ila wana asili ya aidha Rwanda, Zambia, Burundi au Uganda.

Shutuma dhidi ya Katumbi mtandaoni zinazohoji juu ya asili yake kama ni kati ya Muitaliano au Mgiriki zimeibuka kutokana na historia ya mzazi wake wa kiume Ugiriki ambacho kilitawaliwa na Italia, na baadae akahamia mpaka wa kusini mashariki wa Zambia na DRC. Kwa upande wa Mukwege ambae elimu yake ameipata nchini Burundi na Ulaya, kwenye mitandao ya kijamii anaelezwa kuwa ana asili ya Burundi.

Mzazi wake wa kiume alitoka katika kisiwa kilichoko

**DW**

## Ndege ya Kenya yapata hitilafu ikiwa angani

**NAIROBI,** KENYA

SHIRIKA la ndege nchini Kenya, limesema kwamba ndege yake nambari KQ 310 imelazimika kurudi katika kiwanja cha ndege cha Nairobi baada ya kukumbwa na matatizo kwenye magurudumu yake.

Ndege hiyo iliyoruka muda mchache katika kiwanja cha ndege cha Jomo Kenyatta jijini Nairobi, ilishindwa kuendelea na safari yake ya kwenda Dubai baada ya kujitokeza matatizo hayo.

Matatizo hayo yalijitokeza angani majira ya saa tatu usiku baada ya maofisa wa uwanja wa ndege kugundua mabaki ya gurudumu yalithibitishwa kutoka katika ndege hiyo.

Tarifa kuhusu hitilafu kwenye ndege hiyo zilianza kuchapishwa kwenye mitandao ya kijamii ya X na baadhi ya wanahabari nchini humo na kusababisha wakenya wengi kujaa hofu na kuhoji vipi ndege iliondoka ikiwa haijajulikana kuwa na tatizo.

Shirika hilo la KQ lilisema kwamba ndege hiyo ilipofika katika jimbo la Wajir kaskazini mashariki mwa Kenya, rubani wake aliombwa kuirejesha Nairobi na alifanikiwa kutua salama katika uwanja wa JKIA majira ya saa 5:46 usiku.

Uongozi wa shirika hilo uliomba msamaha kwa matatizo hayo na lilitangaza abiria waliokuwemo kwenye ndege hiyo walibadilishiwa ndege iliyoondoka jana.

Hata hivyo, KQ ililazimika kujitetea baada ya vyombo vya habari nchini humo kuelezea malalamiko ya wateja kuhusu huduma zake na hatua za kampuni hiyo kuchelewa kutoa taarifa za kuahirisha safari zake.

**BBC**

## MAKALA

# UHURU WA WANATAALUMA KATIKA MIAKA 62 UHURU WA TANGANYIKA



Na Magabilo Masambu

> Kwanza, nikiri kwamba nchi hii imefika hapa tulipo kwa sababu ya wanataaluma walioshiriki na wanaoshiriki mpaka sasa katika ujenzi wa taifa letu kwenye nyanja mbalimbali ama wamefanya mazuri au mabaya.

TANGANYIKA na sasa Tanzania, imekuwa ikiadhimisha au kusherekea siku ya uhuru kila inapofika Desemba 9 kila mwaka. Kama tunavyofahamu, Tanganyika ilijipatia uhuru wake kutoka kwa Mwingereza Desemba 9, 1961 na baada tu ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, ikaungana na Zanzibar kuunda Tanzania. Kwa hiyo naweza kusema hakuna nchi inaitwa Tanzania iliyopata uhuru mwaka 1961 badala yake ni Tanganyika ama kwa sasa tunaweza kuita Tanzania Bara.

Uhuru uliopatikana ulikusudiwa katika eneo la kiutawala, kijamii na kiuchumi nikiwa na maana kwamba tulipopata uhuru, tulijua tumejikomboa kisiasa kwa maana ya kujitawala, kijamii kwa maana ya fikra za Watanganyika kuondokana na mawazo ya kutawaliwa pamoja na kiuchumi kwa maana ya kuwa na uwezo wa kujitegemea.

Katika madhumuni na malengo yote matatu, sina hakika kama yote yamekidhi haja za Watanzania kwa asilimia 100 baada ya miaka 62 ya uhuru huo.

Leo nataka tutazame kidogo kuhusu kundi muhimu sana la wanataaluma.

Nasema ni muhimu sana kwa sababu tangu kuumbwa kwa dunia, watu wenye maarifa na taaluma mbalimbali wamekuwa wakiaminiwa zaidi na jamii katika kuleta utatuzi wa changamoto mbalimbali kwa kutumia maarifa na taaluma zao.

Lengo ni kuhakikisha tunapata njia mbalimbali za kurahisisha maisha ya mwanadamu. Lakini swali je, katika miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika, wanataaluma nchini wanao uhuru kiasi gani katika kutoa mchango wao wa kitaaluma kwa maendeleo ya taifa?

Kwanza, nikiri kwamba nchi hii imefika hapa tulipo kwa sababu ya wanataaluma walioshiriki na wanaoshiriki mpaka sasa katika ujenzi wa taifa letu kwenye nyanja mbalimbali ama wamefanya mazuri au mabaya.

Pamoja na hayo yote, ukweli ni kwamba pamekuwapo na dhana ya wanataaluma ama kukoseshwa uhuru kamili katika kutoa ushauri wa kitaalam au wanataaluma wenyewe kujikosesha nafasi hiyo kwa sababu mbalimbali.

Moja ya sababu ninayoiona ni kwa baadhi ya wanataaluma kuanza kuyatamani zaidi madaraka ya kisiasa na kutoamini kwamba kupitia taaluma zao bado wana uwezo wa kuyajenga maisha yao bila kutegemea siasa.

Moja ya hatari ya wanataaluma kuyapenda zaidi madaraka ya kisiasa kuliko taaluma ni kukabidhi uhuru wao kwa wenye vyama vya siasa. Kama tunavyofahamu, mfumo wa siasa zetu nchini, ukitaka kuwa kiongozi wa kisiasa ni sharti upitie kwenye chama cha siasa au kuteuliwa na wenye chama chao. Kwa hiyo, uwe umepenya mwenyewe ukapata nafasi katika chama, wenye mamlaka na nafasi yako ni wenye chama au ukiwa umeteuliwa na wenye chama, dhamana ya madaraka yako iko mikononi mwao. Wakiamua utakuwa wasipoamua hutakuwa.

Sisemi kwamba siasa haitaji wanataaluma, lakini wanataaluma wakiipenda zaidi siasa shida ipo kwa sababu itawalazimu wawe chawa kama nilivyowahi kueleza huko nyuma katika baadhi ya makala zangu zilizopita, nikieleza athari za chawa kama wanavyoitwa siku hizi.

Moja ya athari ni watu wengi kuwa wanafiki katika nchi na kushindwa kushauri mambo ya msingi kwa kutafuta nafasi za madaraka au kuogopa kuzipoteza walizo nazo.

Ni jambo la hatari sana katika nchi linapokuja suala la kila mtu kufikiria kuwa mwanasiasa na hii ni kwa sababu mishahara na marupurupu ya wanasiasa ni makubwa zaidi kulinganisha na watumishi wengine wenye taaluma kubwa. Mshahara wa Profesa na Mbunge ni sawa na mbingu na ardhi au mlima na kichuguu.

Kwa hiyo Profesa anaweza kuona ni bora awe mnafiki na chawa kuliko kuishi maisha ya tabu huku akiwa amepoteza muda mrefu zaidi akiitafuta elimu.

Kuna haja ya kupitia upya mifumo yetu ya mishahara ili tusiwapoteze wanataaluma ambao wanasarenda uhuru wao kwa wanasiasa ili wapate madaraka ya kisiasa na hatimaye mishahara na huduma bora zaidi, huku taifa likibaki linaangamia kwa kukosa ushauri wa kitaaluma na wanataaluma wenyewe.

Pili, nawashauri wanataaluma na wasomi, unganeni mjadili namna bora ya kuyapata madaraka ya kisiasa yatakayoendelea kulinda uhuru wenu kama wanataaluma. Yaani ukiyapata madaraka hayo unakuwa na uhakika kwamba bado unao uhuru wa kutoa maoni ya kitaaluma bila ya hofu kwa manufa ya taifa.

Mwisho, pamoja na kwamba wanasiasa wana mishahara mizuri na hawataki kuifuta ili keki ya taifa imnufaishe kila mmoja wetu, basi ili kulinda uhuru wenu ni bora kuisubiri siasa iwapende kuliko kuipenda sana siasa.

Mkiipenda sana mkubali kupoteza uhuru wenu wa kitaaluma katika kuzishauri mamlaka.

**0689157789**
**Dar es Salaam-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kama huna pesa usiwe na wivu, tafuta noti, penzi sawa na maua



Na Adam Fungamwango

> Maana yangu ni kwamba mwanamume yeyote aelewe kuwa mwanamke anahitaji matunzo, na mahitaji mengine na msingi wa yote hayo ni pesa, hivyo wajitahidi sana katika suala ya utafutaji.

KUMBE bwana mambo ya pesa kwenye mapenzi yalikuwapo enzi na enzi. Asikwambie mtu kuwa eti wapenzi wa zamani walipendana bila pesa. Hakuna kitu kama hicho.

Pesa duniani ni kiunganisho kikubwa katika mapenzi, asikudanganye mtu. Ila nikisema hivyo, sina maana kuwa pesa ndiyo mapenzi, hapana.

Ni hivi, hata kama mwanamke anampenda mwanamume sana lakini kama itafika wakati hamtimizii mahitaji yake kama vile chakula, malazi, matibabu anakuacha tu.

Kitu ambacho mwanamke yeyote duniani yuko nacho makini ni matunzo, chakula, malazi, vipodozi na kutopoteza haiba, au muonekano mzuri, urembo ambao kwa kiasi kikubwa wakati mwingine anavipata kutoka kwa kipato cha mwanaume au mpenzi wake.

Mambo yakishakuwa magumu, baadhi ya wanawake wanaogopa sana kuchekwa na kuonekana wameishiwa. Hapo ndipo mambo yanapobadilika, mwanaume anaachwa. Si kwa sababu hapendwi bali hawezi tena kumfanya avutie, atetemeshe watu mitaani.

Wanawake wengi huona aibu kukosolewa na wanawake wenzao kuwa wamekwisha, uzuri wote umeondoka, hana kitu amebaki mifupa tu.

Ndiyo maana baadhi ya makabila likiwemo la Kifipa, anapozaliwa mtoto wa kiume, akiwa bado mchanga kabisa, ni lazima ashikishwe upinde na mshale, au kama hakuna utatafutwa mti mwembamba utakaokunjwa ili kufanana na vitu kama hivyo.

Hiyo ina maana mtoto wa kiume ni mtafutaji, hivyo ni lazima utoke uende msituni ukawinde wanyama kwa ajili ya familia.

Wafipa waliamini kabisa kuwa bila kuwinda na kupata chakula kwa ajili ya mke, atakukimbia na kukuacha peke yako.

Huko nyuma tulisikia vineno vya kinadada wa mjini kuwa 'hapendwi mtu, inapendwa pesa tu.' Kina kitu kinachofanana na hicho kwenye kijembe hicho.

Miaka ya 1990, Kalala Mbwembwe, alitunga wimbo uliorudiwa miaka ya karibuni na Papy Kocha unaitwa 'Fanta' ambao una maneno yafuatayo.

"Fanta wangu uliamua kuniacha peke yangu mama kwa ajili ya pesa ha, mwenye pesa, kanipore nawe hee."

Hii inaonyesha tusiwaonee kinadada wa sasa, hata wale wa zamani walikuwa hivi hivi.

"Wala wewe usilipize kisasi kwa hasidi aliyemrubuni mkeo, mwache acheze na pesa, dunia itamchapa, itamchapa viboko, Moyogani ee.."

Huu ni wimbo wa DDC Mlimani Park uitwao 'Shahada ya Uvimilivu', unaomhusu mtu mmoja ambaye alimrubuni mke wa mwenzake. Sina maana kuwa ukiwa na pesa urubuni wapenzi au wake za watu, la hasha, na pia siwatetei wanawake ambao wanawaacha waume zao ambao hawana uwezo hata wa kuwatunza, wakakimbilia kwa wale vibopa.

Maana yangu ni kwamba mwanamume yeyote aelewe kuwa mwanamke anahitaji matunzo, na mahitaji mengine na msingi wa yote hayo ni pesa, hivyo wajitahidi sana katika suala ya utafutaji.

Kufanya kazi ni muhimu kwa mwanamume yeyote yule na kuwakumbusha hata mwanamke akikupenda vipi lakini kama humtekelezei mahitaji yake ya msingi, iko siku isiyo na jina atakuacha tu kwa sababu nilizotaja huko juu.

Uzuri ni kwamba kila mwanamke ana kiasi chake cha mahitaji, nikiwa na maana gharama.

Leo tunaangalia wimbo mmoja uliopigwa na Western Jazz miaka ya 1970 uitwao, 'Sina Wivu', ambao unamhusu jamaa mmoja ambaye kutokana na kutokuwa na pesa ameamua kumwangalia tu mpenzi wake hamuulizi chochote.

Hii hali unaweza kuitaja kuwa ni msongo wa mawazo tu kwa huyu jamaa ambaye mwanzoni alikuwa na pesa za kuweza kumhudunia mpenzi wake, lakini kwa sasa hana hivyo ameamua kuwa mpenzi mtazamaji tu. Mashairi ya wimbo huu ni haya hapa.

"Maneno yako dada nimeyasikia na lawama zako pia una usemi kaka hunipendi, nikikuona na bwana wala sikuulizi, nikikuona na pesa dada sishughuliki, na nguo mpya kwa wingi yote hayo sikudadisi na hapo mwanzoni mwa mapenzi yetu hayakuwa hivyo."

Baada ya jamaa kuchoka, dada akawa anaonekana na pesa, nguo mpya, lakini jamaa hamuulizi alikovitoa. Nadhani hali hii ilimtisha mwanamama, anaona amuulize kwa nini inakuwa hivi wakati huko nyuma alikuwa akishuku kitu tu anakuwa mkali.

Jamaa akaja na majibu yafuatayo kwenye wimbo huu huu wa 'Sina Wivu.'

"Siku unazozisemea dada, kweli nilikuwa najiweza mama, hata wivu mwenzio sina sasa, sababu naelewa sina cha kukupa sasa."

Jamaa akamwambia ukweli kuwa zamani alikuwa ana pesa, anajiweza, lakini kwa sasa hata kama akimuuliza, au akimzuia hana cha kumpa, kwa hiyo anamuacha chochote kinachoendelea kiendelee.

Hizi ni dalili mbaya kwenye mapenzi, wanakoelekea wanaweza kuachana au kuzika tatizo kubwa.

Cha kufanya ni kwamba mwanamume pamoja na uvumilivu alio nao, atafute pesa kwa kufanya kazi au biashara ili aweze 'kummiliki' kama zamani.

Hii inawakumbusha wanaume kuwa uvivu ni adui, watafute pesa kama wanataka nuru, amani na utulivu katika mapenzi.

Kumbe ukiwa huna pesa hata wivu huna. Tafuteni pesa, Marijani Rajab ameshawahi kusema katika wimbo wake mmoja kuwa mke anataka malazi na chakula kizuri na mapochopocho kidogo. Mwanamke ni sawa na maua, yahitaji kupaliliwa na maji kumwagiliwa. Hapo ndipo utakapoona maua yanachanua na wewe kukuvutia.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi kichefuchefu-2

**Na Adam Fungamwangwo**
**(0716 350534)**

KASSIM hakupata usingizi. Akawaza maneno ya dada yake kuwa amrudie Siwatu.

"Hivi huyu dada ana wazimu huyu?"

Akamuwaza Siwatu jinsi alivyomfanyia kiasi kwamba ilimuathiri kisaikolojia na kuanza kuchukia wanawake wote.

Hiyo ikamfanya asiwe na mwanamke yoyote kwa miaka mitatu, kabla ya kuanza uhusiano na Sauda kabla ya kumuoa mwaka mmoja tu baadaye.

Kwake Sauda ni zaidi ya mke. Ni mtu aliyemrejesha kwenye ulimwengu wa utu, na ubinadamu.

Kitendo alichofanyiwa na Siwatu kilimfanya kuwa na mawazo, akaangukia kwenye ulevi uliokithiri.

Akikumbuka siku ambayo alimkuta mchumba wake na yule jirani yake, roho kama ilitaka kumpasuka, halafu baadaye kukombewa vitu vyote vya ndani kabla ya kupotelea kusikojulikana, ilimtia simanzi kiasi kwamba ilibadi kidogo apate kichaa.

Kibaya zaidi jamaa yule Kindemba naye alihama maeneo hayo, lakini wiki chache tu baadaye zikaja taarifa kuwa jamaa huyo na Siwatu wako pamoja, wakaishi pika na kupakua maeneo ya Buguruni kwa Malapa. Hapo alijua kabisa kuwa licha kuishi pamoja, hata samani wanazotumia ni zile ambazo zimechukuliwa na Siwatu ndani kwake.

Kitu hicho kilimfanya si tu kuchanganya, lakini kuwaogopa wanawake na rafiki yake mkubwa alikuwa ni pombe.


Akaapa kutopenda tena maishani mwake. Kama ameumia hivyo moyoni mwake, alihisi kama ikitokea tena mara ya pili akaumizwa, basi anaweza kufa.

Akawa na kazi ya kuulinda moyo wake usijeruhiwa tena kwa mara ya pili kwani sababu inaweza kuwa hatari zaidi kuliko mwanzo.

Siku zote mipango siyo matumizi. Binadamu hupanga, Mungu hupangua. Penzi ni kama ajali, hutokea tu bila kupangwa, kwa yeyote na popote.

Pamoja na kujidhibiti, kutotaka kujiingiza kwenye penzi, na kuwa makini sana, lakini safari hii aliingia kwenye mapenzi kirahisi zaidi kuliko hata mwanzo.

Kwa Siwatu kazi aliifanya. Ilikuwa ngumu mno, lakini kwa Sauda alinaswa kwenye mtego kirahisi sana kiasi kwamba hata yeye mwenyewe kila akikumbuka anabaki anacheka tu.




**"Mwanamke huyu!" Anajiambia mwenyewe na kucheka kimoyomoyo kila akikumbuka jinsi alivyokuwa hataki tena wanawake, lakini akaanguka kwenye penzi kiulaini kama kumsukuma mlevi kwenye utelezi.**

"Mwanamke huyu!" Anajiambia mwenyewe na kucheka kimoyomoyo kila akikumbuka jinsi alivyokuwa hataki tena wanawake, lakini akaanguka kwenye penzi kiulaini kama kumsukuma mlevi kwenye utelezi.

Ilianza kama mzaha hivi. Wakati akitoka kazini alikuwa akipita kwenye eneo fulani pale Ubungo Kibangu ambalo ilikuwa njia ya mkato kutokezea nyumbani kwao.

Anatokea kwenye njia moja ya barabara isiyokuwa na lami, akaingia kwenye kinjia kimoja cha mkato, nyumba ya kwanza, ya pili ya ya tatu anakutana na kinadada watatu wapo barazani.

Anawasalimia. Wanamuitikia. Anavutiwa na mmoja na kumuangalia zaidi. Siyo kama ametoka kumpenda, ila ni kwa alichokuwa akifanya.

Alikuwa amepakata mdoli kama mtoto mchanga. Ilimvutia kidogo.

Siku ya pili hakupita hapo. Alipita kwenye barabara isiyokuwa na lami na kuzunguka. Hakukatisha kama ilivyokuwa jana.

Siku ya tatu alipita hapo. Mida ni ile ile anapotoka kazini, saa 11:00 jioni kuelekea 12:00. Kwa bahati nzuri akamkuta yule dada. Siku hiyo walikuwa wawili tu. Yeye na msichana mwingine. Alikuwa amempakata yule mdoli kama kawaida. Akatabasamu.

Ikawa ndiyo njia yake, hadi wale kinadada wakamzoea na kumchangamkia kila anapopita.

Kila siku nikipita nakukuta umempakata mtoto, sijaona hata siku moja ukimyonyesha au kumnywesha uji."

Wale akinadada waliangua vicheko, kwani hawakutegemea kama yule kaka anaweza kusema maneno yake, lakini wakikubaliana naye kuwa mwenzao huwa hampi chakula mtoto wake.

"Mchoyo huyu. Huyo mtoto anashinda naye mkononi tu hampi nyonyo, wala uji," mmoja wao akadakia na kuzidi kufanya kicheko kizidi miongoni mwao.

Wiki nzima hakupita tena. Siku aliyopita alimkuta msichana yupo peke yake siku hiyo na mdoli wake.

Akamsalimia kama kawaida na utani wa hapa na pale. "Sasa itabidi huyo mtoto apewe jina," akatania.

Msichana alicheka, halafu akamjibu, "Wewe ndiyo tafuta jina la huyu mtoto," akajibu na vicheko vikatawala baina yao.

"Haya nipe muda wa siku tatu, nitafakari jina gani zuri la kumpa mtoto."

Ikapita kama siku nne hivi, Kassim hakupita hapo, siku ya tano alipopita akawa amelipata jina la mdoli.

"Jina lake kuanzia leo ataitwa Matokeo." Jina hilo lilizusha mshangao na vicheko kutoka kwa wale wasichana ambao siku hiyo kwa bahati nzuri walikuwa wote watatu.

"Na kuanzia leo mwenye mdoli tutamwita mama Matokeo." Mmoja wao akadakia baada ya kumaliza kucheka.

"Basi na yeye aitwe baba Matokeo. Si ndiyo katoa hilo jina." Msichana mwenye mdoli naye akachangia.

Tangu siku hiyo, Kassim akipita anaitwa baba Matokeo, huku mwenyewe akimwita yule msichana mama Matokeo.

Baba Matokeo na mama Matokeo. Mambo yakawa hivyo.

Kuna kipindi Kassim alipata safari ya kikazi na kukaa huko mwezi mzima.

Aliporejea na kupita kwa rafiki zake hakuwakuta.

Alishindwa kumuuliza yeyote kwa sababu ni hao watatu tu ndiyo aliwazoea.

Na kwa bahati mbaya hakuwafahamu hata majina. Jina pekee analolifahamu ni mama Matokeo kwa yule dada anayependa kuwa na mdoli muda wote.

Kwa bahati nzuri kesho yake alikutana na mmoja wao njiani. Akamwambia rafiki yake, mama Matokeo anaumwa na amelazwa Hospitali ya Mwananyamala.

Kassim akamwambia kesho asubuhi anakwenda kazini, lakini atawahi kurudi na kupitia moja kwa moja hospitali.

Wakati geti linafunguliwa kuruhusu wagojwa, tayari Kassim alikuwa wa kwanza ndani ya wodi ya wanawake.

Akapata shida kidogo kwa sababu hawajui ndugu wa mgonjwa na hata mgonjwa mwenyewe hajamzoea kivile, kwa sababu mara zote humuona akiwa amekaa barazani.

Alizunguka karibuni akamalize wodi nzima. Ghafla akajikuta anaitwa.

"We baba Matokeo!" Akasikia anaitwa. Nusu acheke, lakini akajikaza na kuishia kutabasamu. Alikuwa mmoja wa rafiki za mgonjwa aliyepachikwa jina la mama Matokeo na yeye mwenyewe.

Akarudi nyuma kwenye kitanda cha mgonjwa. Akawaona rafiki zake wote wawili.

Akakaa kwenye kitanda cha mgonjwa na kumuuliza maswali kadhaa na kumfariji. Mgonjwa alionekana kushangaa na kufurahi kwa wakati mmoja.

Moja ya mambo ambayo aliyoyakuta hospitali ni bili ya pesa za matibabu. Ilikuwa shilingi elfu hamsini, iliyolipwa kwa mchango wa ndugu na jamaa ni shilingi elfu ishirini na tano.

Aliomba cheti na kupelekwa eneo la kulipia. Akaenda kulipa nusu ya pesa iliyobaki.

Ndipo kwa mara ya kwanza alipolifahamu jina la msichana yule alipolisoma kwenye cheti cha mgonjwa. Anaitwa Sauda Rajab.

INAENDELEA JUMAPILI

# GREEN NASIR ATAMBULISHA KAMPUNI

MENEJA wa wasanii mbalimbali wa Bongo Fleva, Nasir Kalwiha, maarufu kama Green Nasir, amegeukia biashara ya usafirishaji katika mkakati wake kukua kiuchumi.

Green Nasir ambaye amewainua wamamuziki wengi nchini kwa kuwasimamia kazi zao, ametambulisha rasmi kampuni yake ya usafirishaji bidhaa inayojulikana Terrace Logistics & Consultancy Ltd.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika Mwenge Dar es Salaam, Nasir amesema pamoja na kuwa mdau wa Bongo Fleva kwa muda mrefu, anafurahia mafanikio ya kampuni yake na ile ya dada yake Blue Pine Logistics Limited inayohusika na uwakala wa forodha kwa kurudisha sehemu ya faida kwa jamii.

"Katika kufanikiwa kwetu kufungua ofisi kuu hapa Mwenge tumeamua kugusa jamii kwa kutembelea kituo cha watoto yatima kutoa msaada pamoja na kuwasaidia wahitaji mbalimbali kutoka kwenye makundi," amesema Nasir huku akiwaomba mashabiki kumuunga mkono msanii wake Miss Greezy ambaye ameingia kumi bora katika shindano la BSS.



# Zari akana kuachana na Shakib

MWANAMITANDAO na mama watoto wa mwanamuziki maarufu Diamond Platnumz, Zari Hassan amesema kufuta picha za mumewe Shakib Cham kwenye kurasa zake za kijamii kunatokana na matakwa ya kimkataba na kampuni anayoifanyia kazi.

Akizungumza kabla shoo yake ya 'Zari the Boss Lady All White Party', amesema uvumi unaoenea kuwa ameachana na mume wake hauna ukweli bali unatokana na ushiriki wake katika kipindi cha runinga cha Netflix.

Zari alisisitiza kuwa maisha yake ya kibinafsi mara nyingi yanaingiliana na chapa ya biashara yake, kwani yeye hujumuisha majukumu mbalimbali.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RAMSDALE ATAKIWA CHELSEA**
CHELSEA inaweza kumsajili golikipa wa Arsenal na England, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 25, baada ya kuthibitishwa kuwa mlinda mlango wa Blues, Robert Sanchez atakuwa nje ya uwanja kutokana na jeraha la goti. (***Talksport***)

**LEWANDOWSKI KUUZWA**
BARCELONA inaweza kumuuza mshambuliaji wa Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 35, msimu huu ili kusaidia kufadhili uhamisho wa kiungo wa kati wa Newcastle kutoka Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 26. (***Football Transfers***)

**MADRID WAMTAKA JOBE**
REAL Madrid inamfuatilia mdogo wake, Jude Bellingham, Jobe baada ya kijana huyo mwenye umri wa miaka 18 kuonesha kuwa na mwanzo mzuri wa soka wa miaka 18 huko Sunderland. (***90Min***)

**WEST HAM FORNALS**
KLABU ya West Ham inatarajia kumuuza kiungo wa kati wa Hispania, Pablo Fornals mwenye umri wa miaka 27 ili kusaidia matumizi yao ya Januari, huku wagonga nyundo hao wakitamani kuwasajili mabeki wawili na mshambuliaji. (***90Min***)

**MORATO ASAKWA SPURS**
TOTTENHAM Hotspur inapanga kumsaka mlinzi wa Benfica, Morato mwenye umri wa miaka 22 baada ya kuwavutia mawakala waliomtazama katika mechi dhidi ya RB Salzburg katika Ligi ya Mabingwa Ulaya katikati mwa wiki. (***Sun***)

**BUONGIORNO AWANIWA**
CHELSEA inajiandaa kwa pambano la pauni milioni 34 na wababe wa Italia Juventus katika kusaka saini ya mlinzi wa Torino, Alessandro Buongiorno mwenye umri wa miaka 24. (***Sun***)

**AARONSON KUREJEA LEEDS**
KIUNGO wa kati wa Marekani, Brenden Aaronson mwenye umri wa miaka 23 anaweza kukatisha mkataba wake wa mkopo pale Union Berlin na kurejea katika klabu yake mama ya Leeds United Januari. (***Teamtalk***)

**HINCAPIE AWA LULU UKAYA**
LIVERPOOL inakabiliwa na ushindani kutoka Newcastle United, AC Milan na AS Roma kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Ecuador na Bayer Leverkusen, Piero Hincapie mwenye thamani ya pauni milioni 60. (***Bild***)

**TEN HAG BADO MAN**
KLABU ya Manchester United haitafanya uamuzi kuhusu mustakabali wa Erik ten Hag hadi mkataba wa uwekezaji wa Sir Jim Ratcliffe ukamilike, hata kama watafungwa na Liverpool leo Jumapili. (***Football Insider***)

**MODRIC KUONDOKA MADRID**
MCHEZAJI Luka Modric anatarajiwa kuondoka Real Madrid mwisho wa msimu huu kwani klabu hiyo haitarajiwi kutoa ofa ya mkataba mpya kwa kiungo huyo wa zamani wa Croatia mwenye umri wa miaka 38. (***Sport***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DE BEEK KUTUA EINTRACHT FRANKFURT

### ●●●United yakubali kumtoa kwa mkopo kiungo huyo kwenda Ujerumani mpaka......

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imefikia makubaliano na Eintracht Frankfurt kumtoa kwa mkopo Donny van de Beek, kwa mujibu wa ESPN.

> **Van de Beek anataraji wa kujiunga na kikosi hicho cha Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, hadi mwisho wa msimu huu.**

Mkataba huo hauwezi kukamilika hadi dirisha la usajili la Januari litakapofunguliwa na hadi wakati huo kiungo huyo wa kati wa Uholanzi atabakia kuwa sehemu ya kikosi cha kwanza cha United.

Kuna nafasi anaweza kuhitajika dhidi ya Liverpool leo Jumapili huku kocha Erik ten Hag akiwa bila wachezaji kadhaa wa kati wakiwemo Bruno Fernandes, Casemiro, Christian Eriksen na Mason Mount.

Scott McTominay, Sofyan Amrabat, Kobbie Mainoo na Van de Beek ndio viungo pekee wakubwa wako fiti kwa mchezo wa leo pale Anfield.

Van de Beek, ambaye alipatikana kwa uhamisho wa majira ya joto, hajakuwa sehemu ya mipango ya Ten Hag msimu huu.

Kwa mujibu wa ripoti, Eintracht Frankfurt wamepanga kulipa ada ya mkopo na kuna chaguo la kufanya mpango huo kuwa wa kudumu katika makubaliano yao.

Jadon Sancho pia anatarajiwa kuondoka Old Trafford Januari baada ya mzozo wake wa hadharani na Ten Hag.

Mshambuliai huyo wa England hajacheza tangu Agosti na anatakiwa na klabu yake ya zamani Borussia Dortmund na Juventus.

# RICE KUONGEZEWA MAJUKUMU ARSENAL




**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amefichua kuwa atakuwa tayari kumchezesha Declan Rice nafasi ya beki kama ikitokea dharura.

Rice anayecheza nafasi ya kiungo amekuwa moja ya usajili bora wa Arsenal baada ya kununuliwa kwa pauni milioni 105 kutoka West Ham.

Kiungo huyo amekuwa na mchango mkubwa kwenye dimba la kati katika mbio za kuwania ubingwa msimu huu 2023/24, pamoja na Ligi Mabingwa Ulaya baada ya kufuzu raundi ya 16 bora.

"Tuna uhaba wa mabeki, nataka nijaribu kama jambo likitokea, nawezaje kutatua, nadhani alicheza vizuri dhidi ya PSV, aliwahi kucheza nafasi ya beki," alisema Arteta.

"Tunatakiwa kujaribu kama ikitokea dharura, kwanza tuwe na uhakika kama ataweza kuziba hilo pengo, ni mtulivu sana anapokuwa na mpira, anakaba vizuri."

Rice alicheza nafasi ya beki dhidi ya PSV akitokea benchi akichukua nafasi ya William Saliba akiisaidia Arsenal kumaliza kileleni kwenye kundi lao.

Arsenal bado imeendelea kuwakosa Jurrien Timber na Takehiro Tomiyasu kutokana na majeraha huku Arteta akiwapanga Ben White na Jakub Kiwior upande wa pembeni.




# Guirassy agombewa Ujerumani, England

**DORTMUND,** Ujerumani

KLABU za Borussia Dortmund na Newcastle United zimeingia kwenye mbio moja za kuwania saini ya mshambuliaji wa Stuttgart, Serhou Guirassy ambaye hadi sasa amefunga mabao 16 tangu kuanza kwa Ligi Kuu nchini Ujerumani msimu huu 2023/24.

Nyota huyo wa kimataifa wa Guinea mwenye umri wa miaka 27, awali alitajwa kuwa kwenye rada za Brentford ambayo inamtaka akawe mbadala wa Ivan Toney, vilevile Manchester City, Man United na Newcastle United pia zinamtaka.

Inaelezwa kuwa Guirassy ambaye mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika mwaka 2026, ana kipengele ambacho kinamruhusu kuondoka ikiwa timu inayomhitaji italipa euro milioni 30.

Hadi sasa mchezaji huyu hajaweka wazi ikiwa anaondoka au atabaki hadi mwisho wa msimu ingawa timu nyingi zimeonyesha mpango wa kutaka kumchukua.

Mbali ya mabao 16 aliyofunga kwenye Bundesliga, pia amefunga mabao mawili kwenye mechi za kombe la DFB-Pokal.

# Ange: Spurs kusajili beki Januari

**LONDON,** England

ANGE Postecoglou amefichua kusajili beki mpya wa kati ndio kipaumbele cha Tottenham Hotspur katika dirisha la usajili la Januari.

Spurs walianza vyema msimu huu, wakishinda michezo nane kati ya 10 ya kwanza ya Ligi Kuu England na kuwa kileleni mwa msimamo, lakini mfululizo wa michezo mitano bila ushindi uliambatana na majeraha kwa wachezaji kadhaa muhimu.

Postecoglou alishuhudia timu yake ikipata ushindi mnono wa mabao 4-1 dhidi ya Newcastle United Jumapili iliyopita timu ambayo pia ilikumbwa na majeraha lakini bado ana uhaba wa wachezaji kama Micky van de Ven, James Maddison na Rodrigo Bentancur wakiwa nje ya uwanja.

"Unapofikiria juu yake, tulimwacha Davinson Sanchez aende baada ya dirisha kufungwa," alisema Postecoglou akiiambia Sky Sports.

"Kwa namna fulani tulijua tulikuwa tunajihatarisha kidogo, hatukuweza kupata beki wa kati wa ziada ambaye tulikuwa tukijaribu kumtafuta,"

"Lakini mara tulipompoteza Micky (van de Ven) na Eric Dier alikuwa na matatizo pia, hatuna beki mwingine wa kati.

"Ash Phillips ni mchanga, kwa hiyo ni sawa kusema kwamba hatuwezi kukimbia hatari ya kutokea tena, kwa hivyo ni wazi kwamba ni kipaumbele kwetu Januari kusajili beki wa kati, lakini lazima tupate mtu sahihi. Siyo tu kuhusu kuleta mtu mwingine, ni kuhusu kupata yule anayefaa na kwa matumaini hilo litatokea", alisema Ange.

90min majuzi ilifichua kuwa beki wa Everton, Ben Godfrey yuko juu kwenye rada za uhamisho wa Spurs, huku pia akionesha nia ya kumtaka mwenzake Jarrad Branthwaite, wakati Koki Machida wa Union Saint-Gilloise ni mchezaji mwingine aliyevutia timu ya skauti ya klabu hiyo.



HABARI MICHEZO

## Haalubono awafungia kazi washambuliaji Yanga Princess

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga Princess, Charles Haalobono amekiri kuwa safu yake ya ushambuliaji ina mapungufu na sasa ameifungia kazi kuiweka sawa kujiandaa na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Haalubono alisema michezo miwili ya Ngao ya Jamii waliyocheza dhidi ya Simba na Fountain Gate Princess imewasaidia kuona mapungufu ya kikosi chake.

Alisema kazi kubwa anayoifanya ni kusahihisha makosa yao ikiwemo safu yake ya ushambuliaji ambayo imekuwa ikipoteza nafasi nyingi za kufunga.

"Katika mechi mbili tulizocheza kwenye Ngao ya Jamii tulicheza vizuri lakini tukashindwa kutumia nafasi tulizozitengeneza na kufanya kwenda kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti kwa sasa tunafanyia kazi mapungufu haya ili ligi itakapoanza tuwe kwenye kiwango bora," alisema Haalubono.

Alisema, kwenye kikosi chake amekosa namba tisa asilia lakini anawaandaa washambuliaji aliokuwa nao kikosini kwa sasa kuhakikisha wanakuwa kwenye ubora sahihi kuweza kuwapatia mabao.

"Nataka kuwa na timu yenye ushindani mkubwa, ligi haitakuwa nyepesi na tumeona dalili yake kwenye michezo yetu ya Ngao ya jamii hivyo lazima tujiandae vizuri katika kipindi hiki kilichobakia," alisema.

Yanga Princess itaanza kufungua pazi la ligi hiyo wakiwa ugenini dhidi ya Baobab Queens, mchezo utakaochezwa Desemba 21, mwaka huu kwenye uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma.

# BENCHIKHA: SAFU ULINZI IMEIMARIKA ASILIMIA 70

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Simba, Abdelhak Benchikha amesema anaridhishwa na uimara wa safu yake ya ulinzi ambayo anaona imeimarika kwa asilimia 70 mpaka sasa kulinganisha na alivyoikuta wakati akichukua mikoba ya kuifundisha timu hiyo.

Katika mechi mbili ambazo ameiongoza timu hiyo tangu kuchukua nafasi ya Roberto Oliviera 'Robertinho', Simba imeruhusu bao moja pekee kwenye kipigo cha bao 1-0 nyumbani kwa Wydad Casablanca kwenye mchezo wa Ligi ya mabingwa Afrika, lakini iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar juzi kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Benchikha amewapongeza wachezaji wake hasa safu ya ulinzi kwa kuonyesha mabadiliko makubwa ya kiuchezaji.

Akizungumza jana siku moja baada ya mchezo wao dhidi ya Kagera Sugar, Benchikha alisema ameridhishwa kuona timu yake haijaruhusu goli kwenye mchezo wa juzi na kwamba walikuwa na nafasi ya kupata ushindi mkubwa zaidi lakini wameangushwa na uwanja ambao haukuwa rafiki na kuwanyima nafasi ya kucheza soka safi lakini hata hivyo amefurahishwa na kile wachezaji wake walichokifanya.

Alieleza kuwa Kagera ni timu nzuri na walitoa ushindani mkubwa lakini wao walikuwa bora katika kila eneo ikiwemo safu ya ulinzi ambayo hawajaruhusu wapinzani wao kupata bao na kufanikiwa kuibuka na ushindi huo.

"Tulicheza vizuri sana.., nawapongeza wachezaji wangu, tulimiliki sehemu kubwa ya mchezo lakini uwanja haukuwa rafiki na kutunyima kucheza soka safi, Kagera ni timu nzuri wanacheza soka safi na walitupa ushindani mkubwa ingawa sisi tulikuwa bora ndio maana tumepata ushindi," alisema Benchikha.

**Aliongeza kuwa ameridhishwa na jinsi safu yake ya ulinzi kuwa makini na anaimani kubwa kwenye mchezo dhidi ya Wydad Casablanca watafanya vizuri na kuibuka na ushindi ambao kwao ni muhimu.**

"Baada ya mechi hii tunaenda kucheza mechi ya ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca, kwetu ni fainali kwa sababu tunahitaji ushindi, tunarudi uwanja wa mazoezi kujiimarisha zaidi," alisema Benchikha.

Aidha, aliwataka mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi Jumanne kushuhudia na kuisapoti timu yao kwenye mchezo dhidi ya Wydad Casablanca na amewahakikishia wamejiandaa vya kutosha kwa ajili ya mchezo huo muhimu.

"Mpira ni mashabiki, kwetu wa nafasi kubwa sana katika kutusaidia kufanya vizuri, tunaomba wajitokeze kwa wingi na tutaonyesha soka safi zaidi ya lile tulilolionyesha Morocco, tunaka ushindi tu," alisema Benchikha.

Simba inahitaji ushindi pekee kwenye mchezo huo utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa ili kufufua matumaini ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.




Beki wa Simba, Shomari Kapombe (aliyekaa chini), akijaribu kumdhibiti beki wa Kagera Sugar, wakati wa mchezo wa ligi kuu uliofanyika katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi, Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KMC yalia kutokuwa na bahati mechi za Dar

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imesema kuwa inatafuta sababu ya kwa nini hawapati matokeo mazuri wanapocheza mechi zao jijini Dar es Salaam tofauti na wanapocheza ugenini.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Khalid Chukuchuku amesema wamebaini wanakumbana na wakati mgumu wanapocheza mechi zao kwenye viwanja vya Dar es Salaam ambapo wamepoteza mechi nyingi tofauti ya zile walizocheza wanapokuwa kwenye viwanja vya ugenini.

"KMC msimu huu hatujapoteza mechi yoyote nje ya Dar es Salaam, lakini shida inakuja pale tunapocheza Dar tu, wachezaji wanakuwa na presha sijui kwa nini..., kwa sasa tunajiuliza na tunatafuta ufumbuzi ni kitu gani tufanye ili tuondokane na hilo, tukifanikiwa basi timu itafanya vyema msimu huu kwa sababu tunaisaka nne bora," alisema Chukuchuku na kuongeza.

"Angalia hata mechi ya mwisho tuliyocheza na Singida Fountain Gate kule Karatu tulicheza vizuri tu tukafanikiwa kupata pointi moja ambayo kwetu ni muhimu mno, " alisema Chukuchuku.

KMC haijapoteza mechi yoyote ikicheza ugenini ambapo mpaka sasa inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikishinda mechi tano, sare tano na kupoteza tatu, huku zote ikipoteza jijini Dar es Salaam.


Ilichapwa mabao 5-0 dhidi ya Yanga, Agosti 23 mwaka huu, ikafungwa mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji Novemba 3, kabla ya kubugizwa tena mabao 5-0, Desemba 7 mwaka huu dhidi ya Azam FC.

Timu hiyo inatarajia kushuka tena dimbani jijini Dar es Salaam kucheza dhidi ya Simba, Desemba 23.

# Michezo

Jumapili Desemba 17, 2023

Nipashe

## Van de Beek kutua Frankfurt

UKURASA 21

# VAR rasmi kutumika Ligi Kuu Bara

### ●●● CAF yaipa TFF vifaa hivyo na tayari wataalam wa mfumo huo wametua nchini kuanza....

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

RASMI Tanzania inatarajia kuanza kutumia teknolojia ya usaidizi wa kutambua matukio mbalimbali mchezoni (VAR), kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Pamoja na vifaa hivyo kupokelewa nchini, wataalamu kutoka CAF waliwasili nchini juzi, kwa lengo la kukagua baadhi ya viwanja na kufunga VAR.

Akizungumza jana katika mkutano mkuu wa 18 , Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF),Wallace Karia, alisema Tanzania imepokea vifaa hivyo kutokana na uhusiano mzuri kati yake na CAF.

**Karia alisema VAR zitafunga wa pia katika baadhi ya viwanja ambavyo miundombinu bora itakuwa imekamilika na vitatangazwa baadae.**

Alisema anaomba kamati ya waamuzi kushirikiana na wataalamu waliokuja nchini na kuwa tayari kupokea mafunzo, kutoa mafunzo ya matumizi ya vifaa hivyo.

Kufungwa kwa VAR katika viwanja nchini, huenda ikasaidia kupunguza au kuondoa malalamiko mbalimbali yanayotokea katika michezo mbalimbali hasa ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Karia alisema Tanzania itaendelea kuziandaa na kupeleka timu za Taifa katika michuano mbalimbali lengo likiwa kupata nafasi ya kufuzu fainali mbalimbali.

Rais huyo alisema TFF itaziandaa, kusimamia na kutoa kipaumbele kwa timu za taifa za vijana kuanzia umri wa miaka 15 na mkakati wa awali ni kuanza mapema maandalizi.

Alisema TFF itashirikiana na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kuangalia na kupanga timu gani zitaandaliwa kwenda katika mashindano.

Pamoja na hayo, Karia alisema TFF na ZFF zitaendelea kuandaa na kushiriki katika michuano mbalimbali na kuipa Tanzania nafasi ya kufuzu.

"Tukiziandaa timu za vijana na kuzipa nafasi ya kushiriki katika michuano mbalimbali, timu zetu zitakuwa imara, bora na kufanya vyema katika mashindano, tunataka Tanzania ifuzu mara kwa mara kwenye mashindano makubwa ya CAf na hata yale ya FIFA", alisema Karia.

Wakati huo huo Karia amemteua, Sarah Chao kutoka Manyara kuwa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji kwa kipindi cha miaka miwili aliwahuisha Said Soud, Ahmed Mgoyi, Athumani Nyamlani na Hawa Mniga kuendelea katika ujumbe wa kamati hiyo ya juu ya TFF.

# Kuna Aziz Ki mmoja tu Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWa wa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania bara, Yanga jana waliendeleza ubabe wao kwenye Ligi Kuu baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Mtibwa Sugar huku kiungo wake mshambuliaji, Stephane Aziz Ki akijiimarisha kwenye msimamo wa wafungaji wenye mabao mengi baada ya kuifungia timu yake mabao mawili.

Mabao ya jana ya nyota huyo wa Burkina Faso yanamfanya kufikisha idadi ya mabao tisa akiwaacha Jean Baleke wa Simba na Maxi Nzengeli kwa mabao mawili ambao alikuwa akilingana nao kwa idadi ya mabao kabla ya mchezo wa jana.

Ushindi huo wa jana wa Yanga ni kama umetuma salamu kwa Azam FC wanaoongoza ligi kwa tofauti ya pointi moja tu huku Yanga wakiwa na michezo miwili zaidi mkononi kulinganisha na vinara hao.

Wakati Aziz Ki akitupia mabao hayo mawili, mshambuliaji Mzambia, Kennedy Musonda alifunga bao moja likiwa ni la tatu kwenye mchezo huo lakini ni bao lake la tatu msimu huu kwenye ligi.

Naye mchezaji mwenye mbwembwe nyingi, raia wa Afrika Kusini, Mahlatse Makudubela 'Skudu', alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na kufanikisha ushindi huo wa mabao 4-1.



Kwa matokeo ya jana Yanga imefikisha pointi 27, moja tu nyuma ya Azam F, lakini ikiwa na mechi mbili mkononi, imecheza mechi 10 huku Azam ikiwa tayari imecheza michezo 12 na kukusanya pointi 28.

Mtibwa Sugar nayo baada ya kupokea kipigo hicho imeendelea kuburuza mkia ikiwa na pointi tano baada ya kucheza michezo 13 mpaka sasa.

Kilichobadilika zaidi kwenye mechi ya jana ni idadi ya mabao kwani Yanga imefikisha mabao 30, ikizidiwa bao moja tu na Azam yenye mabao 31.

Aziz Ki alianza kufunga bao la kwanza sekunde chache tu kabla ya kwenda mapumziko kwa mkwaju wa penalti.

Penalti hiyo ilitokana na beki Oscar Masai kumfanyia madhambi Clement Mzize aliyekuwa anakwenda kuonana na golikipa wa Mtibwa Sugar Mohamed Makaka.

Aziz Ki alipachika bao la pili dakika ya 65 baada ya kupokea mpira kutoka winga ya kulia, akampa 'msuli' kiungo wa Mtibwa Sugar Said Kazi na kumtoka Oscar Masai kabla ya kugeuka na kuupiga mpira kwa mguu wa kushoto kulia kwa kipa Makaka na ukajaa wavuni.

Mabao yote mawili aliyofunga jana alifanya hivyo kwa mguu wa kushoto na kutimiza idadi ya mabao sita, aliyoyafunga kwa mguu huo, matatu aliyafunga kwa kutumia mguu wa kulia.

Musonda aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Mzize, alifunga bao la tatu dakika ya 76 kwa ustadi mkubwa, kwani pamoja na kwamba mpira ulikuja akiwa ndani ya boksi lakini akiwa anaangalia langoni kwake, aligeuka ghafla na kuachia shuti kali la mguu na kushoto lililokwenda moja kwa moja wavuni, huku kipa Makaka akiwa hajajiandaa kuudaka mpira huo.

Skudu alipachika bao la nne dakika nane kabla ya filimbi ya mwisho lakini wakati kila mmoja akiona mechi hiyo ikimalizika bila Yanga kuruhusu bao, Seif Karihe aliyeingia kipindi cha pili aliifungia Mtibwa bao la kufutia machozi kwa shuti la juu alilolipiga akia mbalina lango la Yanga huku kipa Djigui Diarra akiwa ametoka kidogo langoni.

Karihe aliingia katikati ya kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Matheo Antony.

Katka mechi ya jana, Yanga ilifanya mabadiliko mengi ya wachezaji kadhaa ambao hawajaonekana kwa kipindi kirefu, kama vile Skudu aliyeanza, Cripin Ngushi aliyeingia kuchukua nafasi ya Jesus Moloko, Gift Fred aliyechukua nafasi ya Bakari Mwamnyeto, na Farid Mussa aliyeingia kuchukua nafasi ya Maxi Nzengeli huku Pacome Zouzoua naye akiingia kuchukua nafasi ya Nickson Kibabage.

Katika mchezo huo wa jana, Yanga alimiliki zaidi mpira huku wakipiga kona 10 langoni mwa Mtibwa ambazo hata hivyo hazikuzaa matunda.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >